# Nipashe

Jumanne Desemba 1, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580416

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



Nipashe
TESA
Jumanne Desemba 1, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Kupandikiza uroto kunaweza kuwa tiba VVU
WARAKA KWA SERIKALI
Udhibiti mimba shuleni 'unasahauje' uchunguzi wa maambukizi ya VVU?
ELIMU
NA MWANDISHI WETU
DAUDI MWIGAMBA
• Ana kipaji cha kipekee, hujibu kila swali 'fasta'
• Anajua wakuu, mataifa, miji mikuu duniani

UKURASA 11

**Muuguzi** kortini madai kuomba rushwa 200,000/- kwa mgonjwa

UKURASA 5




**Jela** miaka miwili kumkata viwembe mtoto wa kambo

UKURASA 8

# Mapya sakata wabunge Viti Maalum CHADEMA

• **Hoja** yatolewa kuwasaka walioshiriki hujuma, Ndugai aibua mengine, kina Mdee kuzungumza leo... *Endelea ukurasa 2*


Ester Matiko


Sophia Mwakagenda


Salome Makamba


Halima Mdee


Ester Bulaya



Mbunge wa kuteuliwa Humphrey Polepole (kushoto), akiapishwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai, jijini Dodoma jana. Mwingine aliyeapa ni Riziki Lulida, ambao waliteuliwa na Rais John Magufuli mwishoni mwa wiki. **Habari Uk. 3. PICHA: BUNGE**

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

**SIKU YA UKIMWI: 'MSIACHE ARV KWA MADAI YA KUOKOKA'**

WATU walioambukizwa Virusi Vya Ukimwi (VVU) na wenye maradhi ya...

## PM amaliza mgogoro ardhi Kilosa

UKURASA 3

## Serikali yaanika sababu kasoro majina kwenye ajira za walimu

UKURASA 3





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** **SVEN: BADO DAKIKA 90 CAF** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Kina Halima Mdee kufunguka leo

**Na Enock Charles**

WABUNGE 19 wa Viti Maalum wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) waliofukuzwa uanachama wa chama hicho hivi karibuni, leo wanatarajia kuzungumza kupitia mkutano na waandishi wa habari.

Wabunge hao ambao CHADEMA imewafukuza kwa madai ya usaliti, wanatarajia kutumia mkutano huo kujibu mapigo dhidi tuhuma zinazotolewa dhidi yao.

Taarifa iliyosambaa katika mitandao ya kijamii na kuthibitishwa na Mbunge Ester Bulaya, imeeleza kuwa mkutano huo na waandishi wa habari unatarajiwa kufanyika Mikocheni jijini Dar es Salaam asubuhi.

Mkutano huo na wanahabari ni wa kwanza tangu kutangazwa kwa uamuzi wa kuwafutia uanachama wao na Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, Ijumaa baada ya kikao cha Kamati Kuu kilichofanyika jijini Dar es Salaam kwa kile kilichoelezwa ni usaliti na kukiuka taratibu za chama, baada ya kuapishwa kuwa wabunge wa viti maalum.

"Kwa mujibu wa kifungu cha 6.5.1 d Kamati Kuu imeazimia kuwavua uanachama wanachama wake wote wanaodaiwa kula kiapo cha ubunge wa viti maalum tarehe 24 Novemba 2020," alisema Mbowe.

Wabunge hao ni Halima Mdee, Grace Tendega, Ester Matiko, Cecilia Pareso, Ester Bulaya, Jesca Kishoa, Hawa Mwaifunga, Tunza Malapo, Naghenjwa Kaboyoka, Sophia Mwakagenda na Kunti Majala.

Wengine ni Anatropia Theonest, Salome Makamba, Conchesta Rwamlaza, Agnesta Lambert, Nusrat Hanje, Asia Mohamed, Felista Njau na Stella Fiyao.

Hata hivyo, akizungumza na Nipashe Jumamosi iliyopita kuhusu hatima ya wabunge hao, Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai, alisema bunge hilo litaendelea kuwatambua kwa kuwa bunge bado halijapata taarifa ya kuvuliwa uanachama wao kutoka katika chama chao.

Mbowe alisema mbali na kuvuliwa uanachama wao na Kamati Kuu, pia walivuliwa nyadhifa walizokuwa nazo ndani ya Baraza la Wanawake la CHADEMA (BAWACHA) na mmoja wao katika Baraza la Vijana (BAVICHA).

Mgogoro kati ya wabunge hao na chama ulitokana na madai kuwa walikwenda kuapa bila kufuata taratibu, kwa maelezo kuwa chama hakikuwahi kupeleka majina yao Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ambayo ndiyo yenye mamlaka ya kuyapeleka bungeni.

CHADEMA pia inasisitiza kuwa kiongozi mwenye mamlaka ya kupeleka majina hayo ni Katibu Mkuu, John Mnyika, ambaye anakana kufanya hivyo.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, akizungumza na Balozi wa China hapa nchini, Wang Ke. Mazungumzo hayo yalifanyika katika ofisi ndogo za wizara hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mapya yaibuka wabunge Viti Maalum CHADEMA

**Na Elizabeth Zaya**

SAKATA la wabunge wa Viti Maalum wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) limeibua mapya, baada ya Baraza la Wazee (BAZECHA), Mkoa wa Dar es Salaam, kuishauri Kamati Kuu ya chama hicho, kufanya uchunguzi wa kina wa kubaini wote waliohusika katika mchakato wa kuwapata wabunge hao 19 walioapa hivi karibuni.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, wazee hao walisema wanaunga mkono hatua iliyochukuliwa na Kamati Kuu ya chama hicho ya kuwavua uanachama wabunge hao.

"Tunaunga mkono hatua iliyochukuliwa na Kamati Kuu kwa hawa wasaliti wanaojiita wabunge wa viti maalum, lakini tunaona hiyo haitoshi, tunaomba ufanyike uchunguzi wa kina zaidi kubaini 'virusi' vyote vilivyoshiriki katika mchakato wa kuwapata," alisema Uhuru Kitima, mwenyekiti wa baraza hilo mkoa wa Dar es Salaam.

"Hatutaki kuona tunaendelea kuwa na wasaliti ambao ni virusi ndani ya chama chetu, ni bora wachunguzwe na wachukuliwe hatua kali, hata kama ni vigogo kwa sababu nao ni sehemu ya wasaliti."

Kitima alisema si vema kuacha hata chembe ya watu wa namna hiyo ndani ya chama kwa sababu tayari wamekinajisi chama hicho.

Pia, Kitima alisema baraza hilo limesikitishwa na kulaani vikali kauli iliyotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali juu ya wabunge hao 19 na kwamba wanashangaa kuingilia kazi ya vyama vya siasa wakati yeye siyo mwanasiasa wala kiongozi wa chama chochote cha siasa.

"Tunamshangaa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, yeye siyo kiongozi wa chama wala wa vyama vya siasa, lakini tulimshangaa kutoa tamko la kuzungumzia suala la viti maalum vya akina Mdee na wenzake, na kuingilia uamuzi wa chama utafikiri na yeye kiongozi wa chama," alisema Kitima.

"Tunavyofahamu ni kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali huwa hahusiani na masuala yoyote ya vyama vya siasa, lakini kwa namna ambavyo ameonekana kujihusisha na mambo hayo ya vyama alipaswa kuwa amejiuzulu."

"Na sisi kama wazee wa CHADEMA, tunalaani vikali kauli zake za kujihusisha na mambo ya siasa na ajitafakari, kama ataona inafaa ajiuzulu kwa sababu tunaona nafasi yake haimtoshi."

Alex Makungwa, Mwenyekiti wa BAZECHA Kata ya Mbezi Luis, alikiomba chama hicho kumchukulia hatua Spika wa Bunge, Job Ndugai kwa kuwaapisha wabunge ambao hawakupendekezwa na chama chao.

# Spika: Nitawapangia kazi wabunge CHADEMA

**Na Waandishi Wetu**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema wabunge 19 wa Viti Maalum kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), anawatambua na atawapanga katika kamati za kudumu za Bunge wakati utakapofika.

Ndugai, aliyasema hayo jana, baada ya kuwaapisha wabunge wawili walioteuliwa na Rais Magufuli, Humphrey Polepole na Riziki Lulida.

Alisema kuwa Bunge linawatambua wabunge wote waliokula kiapo na hakuna mtu wakubadilisha hali hiyo, zaidi yao wenyewe kama watataka.

"Kumekuwa na maneno mengi ya kejeli kuhusu hawa wabunge, hali ambayo watu wengine wamejipambanua katika kuliletea dhihaka bunge hili...niwaambie tu wote waliokula kiapo pamoja na wale 19 wa viti maalum nawatambua na siyo Mnyika wala Mbowe wanaweza kubadili hili," alisema Ndugai.

Alieleza kuwa kutokana na mabadiliko ya kikanuni yaliyofanyika, hivi sasa mbunge anaweza kuapishwa hata kama vikao vya bunge havipo.

"Bunge siyo ukumbi tu, hapa tulipo ni bunge pia, hivyo wale ambao wanakejeli naomba niwaonye kuwa hicho wanachofanya siyo sahihi, kwani hivi sasa tumefanya marekebisho ya kanuni kwa kiasi kikubwa," alifafanua Ndugai.

"Haiwezekani kama hawa wabunge waliteuliwa na Rais wasubiri kuanza kufanya kazi za ubunge mpaka pale Bunge litakapo rejea Februari mwaka 2, 2021," alieleza.

Alisema, mabadiliko hayo ni kutokana na utafiti uliofanyika kwa kulinganisha mabunge mengine ya Jumuiya ya Madola.

"Bunge kama Newzeland mbunge hawezi kuingia bungeni bila kula kiapo labda kwa kibali maalum cha bunge, lakini hadi Bunge la Waingereza pia mbunge anakula kiapo kwenye ofisi ya Spika ndipo naingia bungeni," aliongeza Ndugai.

Alisema, hali hiyo inasaidia mbunge kupata fursa ya kula kiapo na kufanya kazi mara moja bila kusubiri vikao vya bunge kuanza.

Aidha, aliwataka Watanzania kuungana kulaani vitendo vya udhalilishaji ambavyo vinafanywa hivi sasa na viongozi wa CHADEMA kwa wabunge wanawake waliokula kiapo kuwa wabunge katika Bunge la 12.

"Naomba nimkumbushe leo hii rafiki yangu Mbowe kuwa, kwa mwanaume wa kitanzania aliyekamilika hapaswi kutukana wanawake hadharani vile haijalishi kosa gani amefanya," alisema na kuongeza:

"Hivi kweli hakumbuki Halima alivyovunjika mkono kwa ajili yake na wengine kupoteza fahamu pia kwa ajili yake?" Alihoji Ndugai.

Ndugai alisema hali hiyo ya kunyanyasa wanawake haitakiwi kufumbiwa macho kutokana tuu na baadhi ya viongozi kuvifanya vyama vya siasa kama kampuni zao.

**AONYA KUWATUMIA MASPIKA WASTAAFU**

Katika hatua nyingine, alivitaka vyombo vya habari kuacha kuwatumia maspika wastaafu kujadili vitu vinavyofanyika hivi sasa bungeni.

**MAJIBU YA CHADEMA**

CHADEMA imesema haiwezi kupeleka barua bungeni kwa sababu hao wanaotajwa hawajawahi kuwa wabunge.

"Tupeleke barua kwani walishawahi kuwa wabunge," alisema Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano wa chama hicho, Tumaini Makene, alipokuwa akijibu swali la Nipashe jana kama wameshapeleka barua rasmi bungeni kulitaarifu kuwa wabunge hao wamevuliwa uanachama.

***Imeandikwa na Paul Mabeja, DODOMA na Elizabeth Zaya, DAR***

HABARI KITAIFA

## Polepole, Lulida waahidi makubwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WABUNGE walioteuliwa na Rais John Magufuli, wameapishwa jana na Spika wa Bunge, Job Ndugai na kuahidi kufanya kazi kwa kujituma ili kumsaidia rais kutekeleza ahadi alizozitoa kwa wananchi wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu 2020.

Wakizungumza baada ya kula kiapo jana katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma, walisema kuwa wanamshukuru Rais Magufuli kuwaamini na kuwapatia nafasi hiyo muhimu ya kuwatumikia wananchi.

Humphrey Polepole, mmoja kati ya wabunge waliokula kiapo hicho, alisema kuwa anamshukuru Mungu kwa kuteuliwa na Rais Magufuli kuwa mbunge katika Bunge la 12.

Aliahidi kufanya kazi kwa kujituma ili kuisaidia serikali kutekeleza ahadi zake ilizitoa wakati wa kampeni.

"Shukrani zangu za dhati ziende kwanza kwa Mheshimiwa Rais kwa kunichagua kuwa mbunge katika Bunge hili la 12, na ninaahidi kufanya kazi kwa nguvu zangu zote ili kuisaidia serikali kufanya maendeleo ambayo nimeahidi kwa Watanzania," alisema Polepole.

Pia, alisema atahakikisha anakwenda kutekeleza yale yote ambayo yapo katika ilani ya chama na atakuwa mbunge mtiifu kwa chama chake na wananchi wote.

Kwa upande wake, Riziki Lulida, alisema anamshukuru Rais kwa kumteua kuwa mbunge katika nafasi zake 10.

"Napenda kumshukuru Rais Magufuli kwa kuniteua kuwa mbunge, lakini shukrani zangu nizitoe kwa familia yangu na wana-Lindi kwa maombi yao ambayo wamekuwa wakiniombea kila siku hadi hii leo nimeapa kuwa mbunge katika Bunge la 12," alisema Lulida.

Alisema baada ya kula kiapo anawaahidi Watanzania kuwa atakuwa mbunge msikivu na kufanya kazi kwa ufanisi ili kuisaidia serikali kutimiza ahadi mbalimbali ilizoahidi.

"Nafasi hii ambayo Rais amenipatia nitahakikisha naifanyika kazi kwa nguvu zangu zote na ninaahidi kuwa sitamwangusha, naomba Mungu anisaidie katika kazi hii ambayo naianza leo," alisema Lulida.

# Serikali yaanika sababu kasoro majina kwenye ajira za walimu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeeleza sababu zilizochangia kuwapo kwa kasoro mbalimbali kwenye majina ya ajira za walimu 13,000 zilizowekwa kwenye tovuti hivi karibu.

Hali hiyo ilizua mjadala na maswali mengi katika mitandao ya kijamii, huku ikibainisha hatua zilizochukulia na zikazochukuliwa kuanzia jana.

Ufafanuzi huo ulitolewa jana na makatibu wakuu watatu kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhandisi Joseph Nyamhanaga, Katibu Mkuu Utumishi, Dk. Laurean Ndumbaro na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo.

Mhandisi Nyamhanga alisema kuwa kutokana na kuwapo kwa maswali mengi katika mitandao ya kijamii kuhusu majina ya walimu waliopata ajira za ualimu, wameshazifanyika kazi baadhi ya dosari.

Alisema maswali ambayo yalikuwa yakihojiwa ni mwalimu mmoja jina lake kujitokeza zaidi ya mara 196, hivyo kuibua mjadala.

"Hili tayari tumeshalifanyia kazi na hii ilitokana na tulivyokuwa tukiandaa orodha hii ili kupandisha kwenye tovuti... kuna tatizo la kiufundi lilitokea, lakini hali hii siyo kama imeathiri lolote au mwalimu huyo kuchukua nafasi za wengine 195, tumeshalifanyika kazi tumeona leo tuwaite ili kuwaeleza suala hili namna ambavyo tumelitatua," alisema Nyamhanga.

Aidha, alisema dosari nyingine mbayo ilikuwa ikilalamikiwa ni majina ya baadhi ya watu waliopata ajira kuonekana ni wahitimu wa kidato cha nne mwaka jana.

"Tayari tumefanya uhakiki kubaini kuwa hii ilitokana na waombaji kukosea kuandika taarifa zao, wengi wao waliandika miaka waliyomaliza kidato cha nne na mwaka waliopata shahada yao basi... lakini ukweli ni kwamba hakuna mhitimu wa mwaka 2019, 2018 wala 2017 aliyechaguliwa kwenye ajira hizi," alifafanua Nyamhanga.

Alisema kwa mujibu wa vielelezo walivyovipitia, kwa waliochaguliwa kupata nafasi hizo ualimu wengi wao ni wahitimu wa kidato cha nne kuanzia mwaka 2010 hadi 2014.

Vile vile, Katibu Mkuu huyo alisema wanaendelea na uhakiki wa majina yote ili kujiridhisha kama ni watu wanaostahili na kuondoa dosali zote.

"Uhakiki huu utaanza leo (jana) na tunatarajia ukamilike ndani ya siku mbili ili watakaostahili waripoti katika maeneo yao na kupatiwa stahiki zao kama ambavyo taarifa ya awali ilivyokuwa inabainisha," alieleza.

Katibu Mkuu Utumishi, Dk. Laurean Ndumbaro, alisema wao ndio wenye mamlaka ya kutoa vibali vya ajira na katika mwaka huu wa fedha, jumla ya walimu 13,000 watapatiwa ajira.

Alisema katika ajira hizo 13,000, walimu 8,000 ndiyo ambao majina yao yametolewa kwenye mtandao na wengine 5,000 watatangazwa baadaye.

Akizungumza kuhusu uhakiki, Dk. Ndumbaro alisema walimu ambao watabainika kuwa wamepata nafasi hizo kwa udanganyifu wataondolewa, na nafasi zao kupatiwa mtu mwingine mwenye sifa.

"Mfumo huu uliotumika kuomba ajira kuna baadhi ya walimu ambao walikuwa ni wa Historia, lakini wamejaza na somo la Hisabati ili mfumo uwatambue," alisema na kuongeza:

"Sasa niseme tu kwa yeyote atakayebainika amepata ajira kwa somo ambalo hajalisomea, ataondolea na kumzuia asipate tena ajira serikalini."



Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini (CCM), Abdulaziz Abood (katikati), akiwa ameshika moja ya mpira wa kuvuta maji na kupata maelezo jinsi unavyotumiwa na baadhi ya wakulima kunyonya maji Bwawa la Mindu kwa ajili ya shughuli za kilimo kinyume cha sheria, alipofanya ziara ya ghafla jana. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA), Mhandisi Tamim Katakweba. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# PM amaliza mgogoro ardhi Kilosa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemaliza mgogoro wa ardhi katika shamba la Chanzuru lenye ukubwa wa ekari 1,598 wilayani Kilosa, Morogoro kati ya Laizer Maumbi na Ameir Nahad, kwa kuagiza likabidhiwe kwa Laizer ili aweze kuliendeleza kwa kulima mkonge.

Hata hivyo, Waziri Mkuu ameagiza eneo wanaloishi wananchi ndani ya shamba hilo kikiwamo kitongoji cha viwanja 60 na Chekeleni, lihakikiwe na kupimwa ukubwa wake na kisha mkulima huyo akafidiwe eneo jingine na wananchi hao wasibugudhiwe.

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo jana katika kikao chake na Makatibu Wakuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Ardhi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, viongozi wa Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Kilosa pamoja na Laizer, kikao kilichofanyika jijini Dodoma.

"Viongozi wa serikali simamieni na mratibu vizuri, ili wananchi wanaoishi katika vitongoji vilivyomo ndani ya shamba hilo wasibugudhiwe waachwe waendelee kuishi na eneo lililobaki lisilokuwa na mgogoro apewe Laizer. Sehemu hiyo iliyopungua Laizer atafutiwe shamba jingine ili kufidia."

Alisema awali shamba hilo lilikuwa linamilikiwa na Sadruddin Rajabali, ambaye alimuuzia Laizer ambaye aliamua kuachana na shughuli za ufugaji na kuanza kulima mkonge, na alipokuwa katika harakati za kubadilisha umiliki shamba hilo liliuzwa kwa mtu mwingine.

Aliwataka watumishi wa sekta ya ardhi wilayani Kilosa wahakikishe suala hilo wanalisimamia vizuri, ili haki itendeke kwa mkulima huyo kukabidhiwa shamba lake na watumishi waliohusika katika mgogoro huo wachukuliwe hatua.

Pia, Waziri Mkuu ameuagiza uongozi wa Mkoa wa Morogoro uhakikishe unabainisha maeneo makubwa yote ambayo hayajaendelezwa na kutoa mapendekezo serikalini.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loatha Sanare, alimshukuru Waziri Mkuu kwa kumaliza mgogoro huo na kuahidi kusimamia utekelezaji wa maagizo na maelekezo yaliyotolewa.

Naye, Laizer ameishukuru serikali kwa hatua iliyofikiwa ya kukabidhiwa shamba hilo ambalo ndilo tegemeo lake kwa sasa, baada ya kuuza mifugo yake yote na kununua shamba hilo ambalo amepanda mkonge.

# Kigugumizi kinavyoweza kutibika - 2

Na Christina Mwakangale

**Katika sehemu ya kwanza ya ripoti hii ilieleza jinsi mtu mwenye kigugumizi anavyoweza kusaidiwa asiteseke na tatizo hilo. Sehemu hii ya mwisho wataalamu wanaeleza jinsi ya kutibu.**

MTU mwenye kigugumizi anaweza kuwa ameikubali hali yake na kuishi katika mazingira yoyote, lakini imani potofu zinawachanganya.

"Imani mbalimbali kwamba kudhani mtu mwenye kigugumizi amerogwa, anapelekwa kwa mashehe au kanisani wengine kwa waganga ni dhana potofu," anasema Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Mtindo Maalum wa Uzungumzaji Tanzania (CHAMMUTA), Ally Abdallah.

"Kuna watu maarufu duniani, waigizaji, wasanii ambao wana kigugumizi na wanaishi kama kawaida."

Kwa mujibu wa Ally, wakati akiwa na tatizo hilo utotoni mama yake alitafuta tiba mbalimbali.

"Mimi nimezaliwa Gerezani, Kariakoo, jijini Dar es Salaam, mama alipojua nina kigugumizi alipata wazo la kuniwekea mkaa chini ya ulimi akiamini nitaacha. Lakini nikaona haina maana zaidi kigugumizi kilibaki palepale," anasema Ally.

### HASIRA

Anasema pamoja na kwamba baadhi husema sababu ya kigugumizi ni hasira, anajitahidi kuepuka.

Mimi huwa nijitahidi kuepuka hasira sababu isije kuwa chanzo najitahidi niwe na furaha muda wote.

Siko katika mahusiano, najua ukiwa peke yako ni rahisi kuwa na furaha muda wote kuliko mkiwa wawili.

### CHAMMUTA

Anasema malengo ya chama ni kutoa elimu shule za msingi kwa sababu ndiko kuliko na mwanzo wa watoto wenye kigugumizi.

Shuleni kuna watoto wanawatania wenzao kwa sababu wana kigugumizi, hii inaathiri watoto.

Watu wengi wenye kigugumizi wanadhaniwa hawana akili wengine wamerudia madarasa kwa sababu darasani hawajamjibu mwalimu maswali yake.

Ally anasema watajitahidi kuongea na waandishi wa habari na wasanii ili kutumia vyema neno kigugumizi.

"Mtu anapokutana na mwenye kigugumizi atambue kwamba tunachosema ni muhimu, kuliko mtindo wa kuongea tunaoutumia. Sababu mtindo uliozoeleka isiwe sababu, kikubwa ujumbe."

### WATAALAMU

Mtaalamu wa Matamshi na Lugha, Rukiya Mohamed kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), anasema katika maadhimisho hayo mwaka huu, lengo ni kukuza uelewa wa jamii kuhusu kigugumizi na kuacha kuwanyanyapaa watu wenye tatizo hilo.

"Maadhimisho yalianza miaka ya 1970 duniani, na kulikuwa na watu maarufu wenye kigugumizi," anasema.

Kitengo hicho anasema kinatoa huduma kwa watoto chini ya miaka mitano hadi saba, wakiwamo watu wazima wenye tatizo hilo.

Kuna wingi wa mahitaji kutoka kitengo hiki MNH na watu walipelekwa kusoma na kuja kusaidia wenye tatizo la kuongea, kumeza na wenye tatizo la kusikia, huduma ilianza 2011.

"Walikuwapo watu wenye wadhifa, walimu, wanariadha walikuwa na kigugumizi na kuona kuna umuhimu kuwa na kitengo hiki," anasema.

### TIBA

Matibabu makubwa wanayopewa wenye kigugumizi wakifika kitengo hicho ni 'therapy' (mazoezi tiba) zaidi, kuliko dawa. Dawa hutolewa iwapo kuna sababu nyingine inayofanya lazima apewe.

"Ili mtu aongee vizuri inahitajika 'breathing' (pumzi), kifua chake kiwe kinakubaliana na maneno, yani pumzi na sauti yake katika koo, inajitajika pumzi ya kutosha ili atoe neno. Utakubaliana na mimi, mfano mtu aliyekimbia sana mwanariadha, mwanamuziki akimaliza kuimba hawezi kujibu vizuri, sababu anakuwa amechoka pumzi ni ndogo."

Ndivyo ilivyo kwa mtu mwenye kigugumizi tunawapa mazoezi ya pumzi namna ya ku-handle breath' (kumudu pumzi) wakati ana 'stuck' (kukwama) ajiandae kuvuta pumzi nyingi ataitoa taratibu atasema neno alilotaka kusema," anasema mtaalamu huyo.

Pia, anasema wanawapa tiba ya kusoma kwa sauti na kufanya mazoezi ya kuwasilisha mbele za watu.

### ATHARI WENYE KIGUGUMIZI

Rukiya anasema watu hao, hutumia nguvu nyingi kuongea, wanakosa kuhudhuria sherehe, kuwa na hofu, kuogopa kuchekwa, wanajitenga, msongo wa mawazo na hukosa furaha.

"Hukosa nafasi sehemu mbalimbali, jamii ibadilike wasione hawa watu kama wana matatizo ya akili.

Wagonjwa wanaongezeka tunapata kutoka ndani na nje ya hospitali hata mikoani.

### DAKTARI BINGWA

Dk. Rachel Mkumbo, bingwa wa masikio, pua na koo, kitengo hicho MNH, anasema kigugumizi humfanya mtu aongee kwa kurudia maneno au kukwama.

"Kuna aina mbili za kigugumizi ni cha utotoni kuanzia miaka miwili hadi sita, umri ambao mtoto anajifunza kuongea.

Anasema kuna watoto ambao akianza shule kinaisha, lakini wengine kinaendelea hadi ukubwani, aina ya pili huanza kwa watu wazima baada ya kupata ajali, mshtuko.

"Watoto wa kiume huwa na tatizo hili zaidi kuliko wa kike, sababu hazijajulikana ingawa wanasema inatokana na 'gene' (jeni) yaani 'genetic' kwamba mtoto anazaliwa nayo," anasema Dk. Mkumbo.



Daktari Bingwa wa Masikio, Pua na Koo, Kitengo cha Matamshi na Lugha MNH, Rachel Mkumbo.

### DALILI

Dk. Mkumbo anasema dalili kwa mtoto, anapata shida anapoanza kuongea kwa kuvuta neno na kurudia au kurefusha sauti.

Anabainisha kwamba iwapo anarudia neno zaidi huwa katika 'pressure consonant' (shiniko la konsonanti) kama vile 'K' na 'G' akitaka kusema, na akitamka kaka atasema kakakkk...au gauni, gagaauni...maneno yote, ana tatizo.

Dk. Mkumbo anasema mwenye kigugumizi huwa na maneno ya ziada kama vile, aaaam, mmmmh huyatumia zaidi.

"Vilevile wanaepuka kuongea kwa kuangaliana 'eye contact' (macho kukutana). Pia huambatana tabia nyingine kama macho kuchezacheza na midomo hutetemeka, wengine mikono huikunja akiongea."

### MWANASAIKOLOJIA

Msaikolojia Tiba, Saldin Kimangale, anasema wenye kigugumizi huwa na tabia ya ukimya na kujitenga.

"Baadhi ya tabia za watu wenye kigugumizi. Hutumia njia ya kuepuka aibu, hatia, kunyanyapaliwa, kukereka na kuepuka fedheha au kudhalilika.

"Hii ni kwa sababu jamii yetu haina uelewa wa kutosha wa namna ya kuishi na mwenye kigugumizi, na hata kiwango cha unyanyapaa bado ni kikubwa kwa sababu hiyo ya uelewa," anasema.

Anasema pia watoto huwatania na kuwaigiza wenzao wenye kigugumizi, bila kujua athari zake kisaikolojia, huku watu wazima wakitumia baadhi ya maneno yanayoashiria unyanyapaa kwa mwenye kigugumizi.

"Ingawa pia wenye kigugumizi hujinyanyapaa zaidi kuliko kunyanyapaliwa, ndio sababu kubwa ya kujitenga na kuamua kunyamaza," anaeleza mwanasaikolojia huyo.

Kimangale anasema uelewa duni wa mhusika na watu wanaomzunguka, una waathiri zaidi kupata ajira.

"Waajiri wengi humuona mwenye kigugumizi kama mtu asiyeweza kuwasiliana, kumbe wanazo mbinu za kuwasiliana vizuri zaidi kuliko vile tunavyojua.

Kwenye mahusiano ya ndoa na familia, ni asilimia saba tu ya watu wamekiri kuwa wanaweza kuwa na uhusiano na mtu mwenye kigugumizi.

Mahusiano hutetereka kwa sababu ya tabia ya hamaki, hasira, msongo, kujitenga ambazo huambatana na ukigugumizi. Sehemu nyingine ambayo wanapata kikwazo ni kunyanyapaliwa na kujinyanyapaa (social and self stigma)," anasema Saldin.

Anasema hali ya uelewa duni huwafanya kukosa fursa mbalimbali za kijamii.

"Wataalamu wanasema kigugumizi huanza kumpata mtu akiwa mdogo kuanzia miaka miwili hadi sita. Kwamba mtu huyo hupata mkwamo wa mawazo au 'thought block'.

"Mwenye kigugumizi hana tatizo lolote la akili wala utendaji, wako sawasawa na mtu mwingine yeyote kitaaluma, kiutaalamu, kiujuzi, mahusiano na kama ipo changamoto ni zile ambazo zinamkumba mtu yeyote hata kama hana kigugumizi."

### UTAFITI

Jarida la 'Knowable Magazine' kwenye makala kuhusu utafiti na sababu za kigugumizi kwenye ubongo, linasema baada ya miaka kadhaa mwishowe utafiti kuhusu tatizo la kigugumizi, linaloathiri mamilioni ya watu duniani, kuna matarajio ya toba.

Gerald Maguire ambaye ni mmoja wa tatizo hilo amaeishi nalo kwa miaka 25.

Maguire ambaye ni mtaalamu wa magonjwa ya akili kutoka Chuo Kikuu cha California, Riverside nchini Marekani, amekuwa akishughulikia shida yake kwa dawa za kuzuia magonjwa ya akili ambazo hazijakubaliwa rasmi kutibu hali hiyo.

"Wamarekani milioni tatu wana kigugumizi. Hiyo ni shida, idadi yao inajumuisha takriban asilimia tano ya watoto, ambao wengi wao huzidi asilimia moja ya watu wazima," anasema Maguire.

Jarida hilo linasema wenye tatizo la kigugumizi ni pamoja na Rais mteule wa Marekani, Joe Biden, mwigizaji James Earl Jones na mwigizaji Emily Blunt.

Ingawa watu hao na wengine wengi, pamoja na Maguire, wamepata mafanikio ya kazi, kigugumizi kinaweza kuchangia wasiwasi wa kijamii na kuteka kejeli au ubaguzi.

Maguire amewatibu wenye kigugumizi na kutafiti matibabu yanayowezekana, kwa miongo kadhaa.

Anasema anapokea barua pepe kila siku kutoka kwa watu ambao wanataka kujaribu dawa, kujiunga na majaribio yake, au hata kutoa ubongo wao kwa chuo kikuu chake, wanapokufa kwa utafiti zaidi.

Anasema anaanza majaribio ya kliniki ya dawa mpya, iitwayo 'ecopipam' baada ya kufanya utafiti mdogo mwaka 2019.

Chuo Kikuu cha Jimbo la Michigan huko East Lansing, kinaeleza kuwa shida za neva zinaweza kusababisha kigugumizi.

Takwimu za mwaka 1991, zinasema, kuna mabadiliko ya mtiririko wa damu kwenye akili za watu wenye kigugumizi.

Mtaalamu wa neva, Soo-Eun Chang wa Chuo Kikuu cha Michigan, anasema ameona kuna tofauti za kimuundo katika kifungu kikubwa cha nyuzi za neva ambazo zinaunganisha kushoto na kulia katika ubongo.

Chang anasema asilimia 80 ya watoto wanaopata kigugumizi wanakuwa na mitindo ya kawaida ya usemi, huku asilimia 20 wakiwa watu wazima.

### NUKUU MITANDAONI

Kwa mujibu wa mtandao wa Wikipedia, mtu mwenye tatizo la kigugumizi anaweza kuathirika hata kumzuia asipate marafiki au kushindwa kuyakabili mazingira na kuzidi kujifungia ndani peke yake.

Mtandao huo unabainisha watu maarufu wenye kigugumizi duniani ambao wamefanikiwa kimaisha kuwa ni mcheza tenisi namba moja duniani, Tiger Woods na Mwanasayansi, Isaac Newton.

Wengine ni Gareth Gates, Notker Balbulus, Bruce Willis, Winston Churchill na Mfalme George VI.

# Walia kulipwa fidia nyumba, mimea

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WAATHIRIKA waliobomolewa nyumba, vibanda na kung'olewa mimea katika mashamba yao wakati wa utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa barabara ya lami kutoka wilayani Tunduru mkoani Ruvuma hadi Mangaka mkoani Mtwara, wameiomba serikali kuingilia kati ili kulipwa stahiki zao wanazodai tangu mwaka 2013.

Aidha, wamesema kuwa wakati viongozi hao wakiendelea kushughulikia kero yao nao pia wanajipanga kutafuta nauli kwa kuuza korosho zao ili waweze kwenda kuonana na mtetezi namba moja wa wanyonge Rais John Magufuli ili kupata ufumbuzi wa kupata haki zao.

Hali hiyo imetokana na wananchi hao kuwa na imani na utendaji wa serikali ya Awamu ya Tano na kuongeza kuwa hali hiyo imetokana na wananchi hao kupigwa danadana kwa muda mrefu na kupelekea baadhi yao kufariki dunia wakiwa hawajapata stahiki zao.

Wakiongea kwa nyakati tofauti kwa niaba ya wenzao Linusi John Mikindani, Gerodi Kosmasi Haule, Mohammed Yahaya Makoti na Abdul Mteko Saidi walisema kuwa hali hiyo imetokana na kuchoshwa na ahadi ambazo zimekuwa zikitolewa na viongozi mbalimbali wakiwamo wakuu wa wilaya ya Tunduru, Chande Nalicho, Agenes Hokororo, Juma Homera sasa Julius Mtatiro, ambao mbali na kuendesha nia ya kuwasaidia lakini juhudi zao bado hazija za matunda hadi leo.

Walisema wakati wakiendelea utekelezaji wa ujenzi huo Julai 31/2017 tume ya watu 8 kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano walifika na kuwatilisha saini kuwa wametumwa na Rais kwenda kuhakiki majina wanaostahili kulipwa na kuwatilisha saini, lakini hadi leo hakuna kinacho eleweka.

Kilichowashangaza zaidi wanasema ni kupokea barua yenye kumbukumbu namba CDA/87/99/01C/148 ya Novemba 2017 iliyosainiwa na Prof. Makame Mbarawa (waziri wa wakati ule) kwenda kwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christine Mndeme, ikieleza kuwa katika kundi la wananchi 477 waliobainika kuwa na vielelezo vinavyo kubalika kati ya 603 waliowasilisha malalamiko yao, kulingana na Sheria ya zamani ya barabara kifungu namba 167 kilielekeza kuwa umbali kutoka katika kati ya barabara ni mita 22.5 ni nyumba moja ya mtu aliyetajwa kwa jina la Geroge Bazoro Kalaliche wa Kijiji cha Lambai ndiye aliye stahili kulipwa fidia hiyo jambo ambalo wanadai kuto kukubaliana nao.

Waliendelea kubainisha kuwa uonevu wanaoutaja dhidi yao umetokana na zoezi hilo kuwa na upendeleo kwani wapo baadhi ya waathirika wenzao ambao pia walipewa 'notice' kutakiwa kubomoa nyumba na kuhamisha mali zao wamekwisha lipwa fidia zao, lakini maeneo yao yalikuwa katika umbali unaofanana.



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wakiendelea na ukarabati wa bomba kubwa la inchi 16 eneo la Vingunguti, lililosombwa na maji kufuatia athari za mvua iliyonyesha hivi karibuni. Kukamilika kwa kazi hii kutarejesha huduma ya maji kwa wakazi wa maeneo ya Kimanga, Kisukuru Chini, Chama, Liwiti, Chang'ombe, Barakuda Ugombolwa, Segerea, Mwembeni, Mpera na Zimbili A. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## SIKU YA UKIMWI

# 'Msiache ARV kwa madai ya kuokoka'

**Na Mwandishi Wetu**

WATU walioambukizwa Virusi Vya Ukimwi (VVU) na wenye maradhi ya ugonjwa huo ambao wameanzishiwa dawa za kufubaza virusi hivyo (ARV) na baadaye kuamua kuokoka, wameshauriwa kutoacha kutumia dawa kwa imani ya kuokoka.

Akizungumza na waumini wa Karmeli Deliverance Ministry International (KDMI), Tangibovu-Mbezi Beach, Dar es Salaam, Mchungaji na Nabii Dk. Enock Mwasambogo alisema, hamuungi mkono mgonjwa yeyote anayeacha kutumia dawa hata kama ameokoka.

Dk. Enock, alisema dawa za ARV zinampunguzia mtu mwenye maambukizi makali ya maradhi hayo na kumfanya aonekane mwenye afya na matumaini wakati wote anapokuwa kwenye maombi akiutafuta uponyaji.

"Ukimwona mgonjwa wa Ukimwi aliyeokoka anatupa ARVs zake wakati hajapokea uponyaji mwambie asiige yasiyoigwa, na wala asijaribu kuonyesha kuwa na imani zaidi hata ya Yesu mwenyewe," alisema.

Alisema ni vyema mgonjwa akaendelea kumeza dawa zake kwa utaratibu ufaao badala ya kuruka dozi.

"Hakuna mahali Mungu alipokataza watu waliookoka wasiende hospitali au wasitibiwe, ndio maana tunahubiri na kuwashauri wagonjwa wanaokuja kanisani wahakikishe hawapuuzi ushauri wa madaktari wakati uponyaji wa Mungu ukiendelea."

"...Wengi wanakufa kwa imani ambazo hata Mungu mwenyewe haziungi mkono. Una malaria, unapewa dawa kunywa umalize dozi usitupe eti kwa kuwa umeokoka, ukicheza utakufa na tutakuzika," alisema na kuongeza kuwa mambo ya rohoni yafanyiwe kazi kiroho na ya mwilini yafanyiwe kazi kwa njia bora za mwilini ili Mungu naye ayabariki.

# Muuguzi kortini madai kuomba rushwa Sh. 200,000 kwa mgonjwa

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora, imempandisha kizimbani mtumishi wa Idara ya Afya katika hospitali ya wilaya hiyo, Mahakama ya Hakimu Mfawidhi Wilaya ya Igunga, Wallace Joseph Kazili, kwa tuhuma za kuomba rushwa ya shilingi 200,000 kutoka kwa mgonjwa.

Mapema Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU Wilaya ya Igunga, Mazengo Joseph, alidai kwamba mshtakiwa, Wallace Joseph Kazili (52), mkazi wa Mtaa wa Masanga, mjini Igunga, alitenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha 15 (1) (a) na (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11 ya mwaka 2007.

Mbele ya Hakimu wa Wilaya ya Igunga, Lydia Illunda, Mwendesha Mashtaka huyo alidai kwamba Oktoba 30, mwaka 2019, mshtakiwa huyo akiwa muuguzi katika Hospitali ya Wilaya ya Igunga, aliomba rushwa ya Sh. 200,000 kutoka kwa Kasembe Bundala Nangale, mkazi wa Wilaya ya Kishapu, mkoani Shinyanga ili kumpatia dawa ya TB ya mtu mmoja aliyemtaja kwa jina la Bugumba Luhende Lisawi, ambaye alikuwa amelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Igunga.

Aidha, mwendesha mashtaka huyo alidai pia kwamba katika tarehe hiyo hiyo, mwezi huo huo, Kazili alipokea kwa njia ya simu shilingi 50,000 kama malipo ya awali ya shilingi 200,000 alizokuwa ameomba.

Kwa mujibu wa mwendesha mashtaka huyo, ndipo Novemba 01, 2019, mshtakiwa huyo alipokea kiasi kingine cha shilingi 50,000 kama malipo mengine ya awali ya shilingi 200,000 hivyo kupokea jumla ya shilingi 100,000 kati ya shilingi 200,000 alizokuwa ameomba.

Hata hivyo, baada ya kusomewa shtaka, alikana, hivyo hakimu kuahirisha kesi hadi Desemba 10, mwaka huu. Mshtakiwa yupo nje kwa dhamana ya shilingi 300,000 za maandishi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua zichukuliwe kuiepusha Tanzania kuwa jangwa

**JANA** katika gazeti hili tulichapisha habari inayotoa tahadhari kwa Watanzania kuwa miaka 40 ijayo, nchi itageuka jangwa, iwapo wananchi wataendelea kuvuna kiholela misitu ya asili na kufanya shughuli mbalimbali za kibinadamu bila kuzingatia matumizi endelevu ya rasilimali hiyo.

Habari hiyo ilieleza kuwa misitu ya hifadhi ya jamii ambayo maelfu ya hekta zake hayajahifadhiwa kisheria, zinateketea kutokana na ongezeko la shughuli za kibinadamu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), Rahma Njaidi, alisema ili kukabiliana na hali hiyo, ni lazima misitu ya jamii ya vijijini ikatengwa na kurasimishwa kwenye ardhi ya vijiji.

Alitoa mfano wa baadhi ya maeneo ikiwamo mikoa ya Morogoro na Lindi, ambayo imetenga maeneo hayo na mafanikio makubwa yameonekana.

Alieleza kwa kina kuwa iwapo misitu itarasimishwa wananchi watashiriki kuhifadhi na kuvuna mazao ya misitu kwa maendeleo endelevu, utaratibu ambao utakuwa na manufaa binafsi, vijiji na taifa kwa ujumla.

Katika habari hiyo, Mkurugenzi Msaidizi wa Shirika la kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania, TFCG, Emmanuel Lyimo, akabainisha utafiti uliofanywa na serikali kupitia Shirika la NAFOMA mwaka 2017 ulibaini hekta 469,000 zinapotea kila mwaka katika misitu iliyohifadhiwa na vijiji.

Aidha, alishauri usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii kwa kuzingatia wajibu wa jamii kuhakikisha wanasimamia misitu na kuwa na haki ya kupanga usimamizi wa misitu na mapato yatakayotokana na mazao ya misitu, ambayo huenda kwa wananchi moja kwa moja.

Tahadhari hiyo ni muhimu sana ili hatua zichukuliwe na wadau wote, kuhakikisha misitu inalindwa na kutunzwa kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

Misitu ni tegemeo la wote na si jamii iliyopo karibu nayo, kwa kuwa hewa safi, vyanzo vya maji vinategemewa kutokana na misitu hiyo, kuondoa hewa ukaa, kwa ajili ya kuni, mkaa, asali na mazao ya misitu.

Misitu ya kijamii ni raslimali ambayo huisaidia jamii kupata kipato, na ndiyo maana vipo vijiji vinapata mapato ya zaidi ya Sh. milioni 100 ambayo hutumiwa na vijiji kufanya miradi ya maendeleo na wanalipwa.

Vipo vijiji ambavyo vinapata fedha kutokana kuwa na misitu ambayo huzalisha hewa safi, eneo limepimwa na wanalipa fedha kutokana na kupunguza hewa ukaa duniani.

Zipo nchi ambazo zina viwanda vingi, ambazo zinachangia uharibifu mkubwa wa mazingira na kuzalisha hewa ukaa ambayo imechangia mabadiliko ya hali ya hewa.

Mabadiliko ya tabia nchi husababisha kubadilika kwa vipindi vya mvua, majanga ya asili kama vimbunga, mafuriko na ukame wa muda mrefu ambao huleta madhara makubwa kwa jamii husika.

Vipo vijiji vimeshindwa kutunza misitu kutokana na kukosa kazi mbadala na kugeukia misitu kama kitega uchumi cha kujipatia kipato kupitia kuuza mbao, kuchoma mkaa na kukata miti ovyo.

Uvunaji wa miti usio endelevu ni tishio kwa uhai wa misitu na matokeo ya yote ni hatari kubwa iliyombele ya nchi kugeuka jangwa.

Tunaona ni wakati sasa wa serikali kushirikiana na wadau kudhibiti hali hiyo, kwamba sasa gesi asili ianze kutumika kwa ngazi ya kaya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Manispaa hii ni chachu maendeleo ya taaluma

**MAKTABA** ni mkusanyiko wa taarifa mbalimbali zenye kuelimisha ambazo zimepangiliwa katika mfumo mahiri zinazotumiwa kujifunza, kufanya rejea, kuburudika na hata utafiti.

Zinaweza kuwa ni maktaba za umma au binafsi, zikimilikiwa na vyuo, shule na tasisi yoyote.

Yanayotarajiwa kupatikana katika maktaba ni mengi kuanzia kuelimisha, kuburudisha, kuonya hadi kuadabisha, lakini nitajikita zaidi katika maktaba za shule za msingi na sekondari na jinsi zinavyoweza kusaidia wanafunzi kuwa mahiri wa taaluma.

Huduma hizo zinatakiwa kuwa mkusanyiko wa vitabu vya ziada na kiada, vya rejea, mihtasari ya masomo, atlasi, hadithi mbalimbali, tasnifu, projekti za wanafunzi, ripoti za utafiti, picha, sinema, majarida, mitihani ya zamani na vielelezo.

Shule kuwa na maktaba ni muhimu kwa maendeleo ya elimu na ni njia inayowapa fursa wanafunzi kujisomea na kupata maarifa zaidi, kwa yale waliyofundishwa darasani na kukuza na kuongeza uelewa kitaaluma.

Aidha, maktaba huboresha malengo ya elimu kwa kuwafanya wanafunzi wapende kusoma na kujifunza na kujua mambo mengi.

Hivyo, walimu na wakutubi wanapofanya kazi kwa kushirikiana, wanafunzi hufanikiwa kujifunza kwa umahiri zaidi, huoongeza uwezo wa kujifunza na kutatua changamoto.

Sera ya kutoa elimu bure kuanzia shule ya awali hadi kidato cha nne, ni utaratibu unaokwenda sambamba na mkakati wa uboreshaji wa miundombinu ya shule ikiwamo ujenzi wa maktaba.

Maktaba hizo ni sehemu muhimu katika mchakato wa ufundishaji na kujifunza, unaompa fursa mwanafunzi kujisomea zaidi akiwa mwenyewe na kujipatia maarifa ya ziada, kwa yale aliyofundishwa na mwalimu akiwa darasani.

Halmashauri ya Musoma mkoani Mara, ni miongoni mwa maeneo ambayo wananchi wamehamasishwa na sasa wanashirikiana na serikali kwenye ujenzi wa maktaba katika shule za msingi na sekondari.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, John Kayombo, anasema, mwitikio huo wa wananchi umechangia kuzifanya baadhi ya shule za msingi kuwa na maktaba za kisasa.

Anatolea mfano Shule ya Msingi Butata, kwamba ni mojawapo na ilijengwa kwa nguvu za wananchi na wadau wengine wa elimu, kwa lengo la kusaidia wanafunzi kujisomea.

"Wananchi wamechangia nguvukazi yao kwa kusomba maji, mchanga, kokoto, mawe na fedha taslimu, kisha wadau wa elimu wakatoa meza kabati,vitabu na vitu vingine muhimu," anasema Kayombo.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, ujenzi wa maktaba unaendelea katika shule mbalimbali kwenye halmashauri hiyo, ili kuwaongezea wanafunzi ari ya kujisomea na kupanua maarifa.

Kimsingi mwanafunzi kupata mazingira bora ya kujisomea, ni chachu ya kujifunza na kumwezesha kuwa na uwezo zaidi wa kuelewa alichofundishwa, hivyo huduma za maktaba haziepukiki.

Maktaba inawezesha wanafunzi kupata muda zaidi wa kujisomea wenyewe na kwa utulivu na urahisi wa upatikanaji wa vitabu unaokwenda sambamba na utunzaji wa vitabu, ili waendelee kuvitumia.

Hivyo halmashauri ama wazazi ambao hawajaona umuhimu wa shule zao kuwa na maktaba, wajifunze kwa wenzao wanaoendelea na miradi ya ujenzi ili shule ziweze kuwa na huduma hiyo.

Wafanye hivyo wakitambua kuwa maktaba ni kiunganishi kati ya wasomaji ama watumiaji na sehemu ambayo inasaidia wanafunzi kuongeza maarifa na uelewa wa mambo mbalimbali ya elimu.

Ikumbukwe kuwa maktaba za shule zina vifaa mbalimbali vinavyotoa taarifa, kuelimisha na kuburudisha na hutoa huduma pia kwa walimu na ni viungo muhimu katika kukamilisha malengo ya elimu ya msingi na sekondari.

Maktaba zinamtayarisha mwanafunzi kuwa raia bora katika jamii na taifa kwa ujumla na humwezesha na kumkuza mtumiaji kuwa na tabia ya kuendelea kujifunza mwenyewe, kuwa na uwezo wa kutafiti, kudadisi, kubuni na kuhoji.

HABARI KITAIFA

# Uharibifu Bwawa Mindu wamshtua Mbunge wa Moro

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MBUNGE wa Jimbo la Morogoro Mjini (CCM) Abdulaziz Abood, amefanya ziara ya kushtukiza katika vyanzo vya maji vya Bwawa la Mindu na kujionea uharibifu ambao unatishia uhai wake, kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu.

Katika eneo hilo kuna shughuli za kilimo cha mazao mbalimbali unaofanywa na wakulima, huku kina chake kikiwa hatarini kupungua na kusababisha uhaba wa maji kwa Manispaa ya Morogoro ambayo inategemea chanzo hicho.

Bwawa hilo ni chanzo kikuu cha upatikanaji wa maji kwa asilimia 75 kwa wakazi zaidi ya 500,000 wa Manispaa ya Morogoro.

Akizungumza na wakazi wa Kata Mzinga, Mindu na Luhungo ambavyo vimezunguka vyanzo vya maji yanachangia ujazo wa bwawa hilo, Mbunge Abood, alisema kilimo hicho kisipodhibitiwa wananchi wa manispaa hiyo watakosa huduma ya maji.

"Rais Dk. John Magufuli ametukumbuka na kutupa mradi mkubwa wa maji, sasa maji hatuwezi kuyapata bila kutunza vyanzo vya maji ambavyo vinaharibiwa na kilimo, hivyo lazima tuwe mabalozi wazuri wa kutunza vya maji tusikubali vyanzo vya maji viharibiwe," alisema.

Aliwashuhudia baadhi ya wakulima wakiendelea na shughuli za kilimo cha nyanya, mahindi, mihogo, mboga, bamia, vitunguu, pilipili, migomba, nyanya chungu na mazao mengine mchanganyiko ikiwamo mpunga.

Akizungumza na wakulima hao, Abood alisema kuwa atakaa na wakulima hao ili kuangalia namna ya kusitisha haraka shughuli hizo za kilimo na kuwatafutia maeneo mengine, ili wakaendelee na shughuli zao za kilimo kwa lengo la kulinda bwawa hilo.

Aidha, aliahidi kuchangia miche 10,000 ya miti kwa ajili ya kupandwa pembezoni mwa bwawa hilo, ikiwa ni kuunga juhudi za kuzuia uharibifu wa mazingira uliotokana na uvamizi wa shughuli za kibinadamu.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MOROWASA), Mhandisi Tamim Katakweba, alisema wamebaini uvamizi wa shughuli za kilimo ndani hifadhi ya bwawa hilo unafanywa na wakulima kutoka mikoa ya Singida, Kigoma, Mwanza na Dar es Salaam.

Alisema wakulima hao ambao wamewaweka wafanyakazi wanaondesha kilimo hicho wakiwa na lengo la kupata mazao ya kufanya biashara kwenye masoko mbalimbali yaliyopo hapa nchini.



Wakazi wa Makong'ondela wakiangalia sehemu ya Mto Nalingwenya ambayo Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) watajenga daraja litakalounganisha vijiji vya Michiga - Makong'ondela, mkoani Mtwara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfanyabiashara adai mahakamani kutotambua vielelezo

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA Ayubu Kiboko, anayekabiliwa na kesi ya kusafirisha dawa za kulevya, amedai mahakamani kwamba vielelezo vyote vinavyodaiwa kukutwa nyumbani kwake havifahamu na kwamba ameviona kwa mara ya kwanza vikitolewa na mashahidi.

Kadhalika, amedai kuwa anapinga kuwa chenga au unga uliokuwa katika mfuko wa nailoni, vikopo viwili vyenye unga mweupe, mfuko mweusi wenye unga mweupe ndani na mfuko unaodaiwa kukutwa kwenye eneo la kutunzia viatu, vyote hivyo ameviona kwa mara ya kwanza mahakamani vikitolewa kama vielelezo.

Kiboko na mke wake, Pili Kiboko, wanaokabiliwa na tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya, jana alitoa ushahidi wa utetezi katika Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa maarufu kama Mahakama ya Mafisadi, iliyoketi chini ya Jaji Lilian Mashaka.

Akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Majura Magafu, alidai kuwa anapinga kuvifahamu vielelezo hivyo na kwamba ameviona kwa mara ya kwanza akiwa mahakamani hapo.

mbele ya Jaji Lilian Mashaka, upande wa Jamhuri uliwakilishwa na mawakili wa serikali Salim Msemo, Constantine Kakula na Candid Nasua.

Alidai kuwa Mei 23, 2018 kati ya saa nane au tisa usiku akiwa amelala nyumbani kwake alisikia mlango ukigongwa kwa nguvu ndipo alipomwamsha mke wake ambaye alishtuka na kelele za ugongaji huo.

Alidai kuwa mke wake alipoamka alichukua silaha yake na kushuka chini akitokea ghorofani kwenye chumba anacholala.

"Mtukufu Jaji, nilichukua silaha yangu na kushuka chini kuwasikiliza waliokuwa wanagonga, nilipofika nikawauliza nani anagonga wakasema ni askari polisi. Nilirudi juu kuchukua funguo kwa kuwa tunalala nayo baadaye nikashuka na kuwafungulia mlango," alidai na kuongeza:

"Nilipofungua mlango askari saba walinivamia na kunirudisha jikoni huku wakinipiga kabla ya kumfuata mke wangu na kushuka naye chini, huku mimi nikiwa nimefungwa pingu, waliniambia wanataka kufanya upekuzi wa nyumba yangu, lakini sikujua wanatafuta nini," alidai Kiboko.

Alipowahoji wanataka nini, walimjibu kwamba wanatafuta dawa za kulevya na chochote chenye kutia shaka, aliwahoji kama wanampekua bila uwapo wa mjumbe, askari hao walimwomba ufunguo wa geti wakatoka na baada ya muda walirudi na mjumbe Christina Macha.

Alidai baada ya mjumbe kufika upekuzi ulianza na walianzia chumbani kwake wakiwa na askari wanne pamoja na shahidi mwingine aliyefahamika kwa jina la Raymond Kimambo ambaye ni jirani wa Kiboko.

Alidai katika upekuzi wote askari hao walikamata bastola moja, kadi nne za benki simu mbili na mafaili yenye nyaraka. Alidai pia walikamata kifuko cha nailoni angavu chenye chenga za mkaa kilichopatikana chumbani kwa msaidizi wa kazi.

Pia alidai baada ya upekuzi askari walijaza fomu ya ukamataji na kuorodhesha vitu vilivyokamatwa kisha wakampatia asaini na wakampeleka ofisi za Mamlaka ya Dawa za Kulevya (DCEA).

Alidai akiwa DCEA Inspekta Ambilikile alimfuata akiwa na bahasha tano ambazo alimwambia zina vitu walivyovikamata asaini kwa ajili ya kupeleka sehemu husika kwa uchunguzi.

Alimaliza utetezi wake kwa kudai kuwa hakubaliani na tuhuma zinazomkabili kwa kuwa upekuzi ulipofanyika hakukupatikana kitu nyumbani kwake.

Aliiomba mahakama kumwachia huru ili aweze kuendelea na shughuli zake kwa sababu tuhuma zinazonikabili sio za kweli.

# China yaipongeza Tanzania uchaguzi mkuu

**Na Mwandishi Wetu**

CHINA imesema itafanya kazi kwa ukaribu na Serikali ya Tanzania baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu, kwa lengo la kuiwezesha kupiga hatua za maendeleo kwa haraka kwa faida ya pande zote mbili.

Hayo yamo katika barua ya pongezi iliyotumwa na Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi, kwenda kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, iliyowasilishwa kwake na Balozi wa China nchini, Wang Ke.

Akizungumza baada ya kukabidhi barua hiyo ya pongezi, Wang Ke, alisema nchi ina imani na Tanzania hususani baada ya uchaguzi mkuu uliomalizika kwa utulivu na amani na kwamba imejipanga kuimarisha uhusiano wa kimkakati, ili kuwaletea wananchi maendeleo.

Kwa upande wake, Waziri Prof. Kabudi, alisema amepokea kwa unyenyekevu salamu hizo za pongezi kutoka kwa Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi, na kuongeza kuwa katika mazungumzo yake na Balozi Wang Ke waliangazia masuala ya kimkakati ya kutekeleza dhamira ya serikali kimaendeleo.

Katika hatua nyingine, Waziri Prof. Kabudi alikutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Sweden nchini, Anders Sjoberg na baadaye kukutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Finland nchini, Riitta Swan na kuzungumzia namna ya nchi hizo zitakavyoendelea kushirikiana katika nyanja za kiuchumi na kijamii.

Alisema lengo ni kudumisha urafiki lakini kupiga hatua za kimaendeleo na kukuza uchumi.

# Madiwani, mbunge kubanwa utatuzi wa kero za wananchi

**Na Marco Maduhu,**

SHINYANGA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Shinyanga Mjini, kimeweka mikakati ya kuwabana madiwani na mbunge kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Shinyanga Mjini, Abubakari Mkadamu, alibainisha hayo jana kwenye kikao cha Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema chama hicho kimeandaa mkataba baina ya madiwani, mbunge na CCM, kusikiliza kero za wananchi pamoja na kuzitafutia ufumbuzi, na kuwasilisha taarifa hizo kila baada ya miezi mitatu kuhusiana na mikutano ya hadhara ambayo wameifanya.

"CCM Wilaya ya Shinyanga Mjini tumeandaa mkakati wa kuwabana madiwani pamoja na mbunge, kupanga siku maalumu za kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi pamoja na kufanya mikutano ya hadhara, na taarifa hizo wawe wanaziwasilisha kwenye ofisi ya chama kila baada ya miezi mitatu," alisema Mkadamu.

Pia, alisema kabla madiwani hao hawajaenda kwenye kikao cha Baraza la Madiwani, wasikilize kwanza kero za wananchi na kuziwasilisha kwenye baraza hilo, na wakitoka waandae tena mkutano wa kuwapatia mrejesho, na kuendelea kutatua changamoto zinazowakabili.

Mbunge Katambi, alisema atakuwa karibu na wananchi kusikiliza kero zao na kuzitafutia ufumbuzi pamoja na kutekeleza ahadi ambazo aliziahidi kwenye kampeni, ikiwamo kutatua tatizo la ajira kwa vijana na kujenga miundombinu ya kiuchumi.

# Jela miaka 2 kumkata viwembe mtoto wa kambo

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kigoma imemhukumu kwenda jela miaka miwili na kulipa fidia ya shilingi milioni tano Agness Damian (40), mkazi wa Mji Mwema, Manispaa ya Kigoma Ujiji kwa kosa la kumshambulia na kumkatakata kwa wembe mtoto wa mume wake mwenye umri wa miaka 15.

Katika kesi hiyo Agness alishtakiwa kwa kosa alilolitenda Juni 18, 2020 kwa kumpiga mlalamikaji akimtuhumu kumpiga mdogo wake ambaye ni mtoto wake.

Mshtakiwa alishtakiwa kwa kufanya ukatili huo ambao ulisababisha mlalamikaji kulazwa hospitali kwa siku nane kwa matibabu kutokana na majeraha aliyoyapata.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Kigoma, Eva Mushi, alisema mahakama imepitia na kuridhishwa na ushahidi wa upande wa mashtaka uliojumuisha mlalamikaji wa tukio hilo, mama mzazi wa mtoto na baba mzazi wa mtoto huyo, jirani, daktari na ushahidi wa polisi.

"Kwa mujibu wa kifungu cha 225 cha sheria ya kanuni ya adhabu sura namba 16 marejeo ya mwaka 2019 mahakama imemtia hatiani na kumhukumu kwenda jela miaka miwili na fidia ya shilingi milioni tano," alisema hakimu.

Kabla ya hukumu mshtakiwa alipotakiwa kujitetea, aliomba kupunguziwa adhabu kwa kuwa yeye ni yatima na ana watoto wawili na kati yao mmoja akiwa na umri mdogo.



Wapita njia wakivuka majitaka yanayotiririshwa kutoka vyoo vya baadhi ya wakazi wa Manzese Kilimani, jijini Dar es Salaam juzi, hali ambayo inaweza kuhatarisha afya za watu. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Benki ya UBA yaiahidi serikali ujenzi miradi

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya UBA Tanzania, imesema itaendelea kuunga mkono ujenzi wa mradi wa umeme wa Rufiji ikiwa ni pamoja na kuhakikisha inapeleka huduma za kifedha karibu na mradi huo.

Akizungumzia wakati wa kufungua tawi jipya katika eneo la mradi huo, Mkurugenzi Mtenda wa benki hiyo nchini, Kingsley Ulinfun, alisema lengo ni kuhakikisha wanaoshiriki katika mradi huo wanapata huduma karibu na kuwapunguzia usumbufu wa kwenda mbali.

Pia alisema benki hiyo ina mpango wa kufungua matawi mengine matano Visiwani Zanzibar, Mwanza pamoja na mikoa ya Mbeya na Arusha.

"Kufuatia kuiunga serikali mkono katika mradi wake huu muhimu kwa taifa la Tanzania kwa kutoa dhamana ya Sh. milioni 400 kwa ajili mradi huu wa umeme wa Rufiji, UBA Tanzania imeendelea tena kuunga mkono mradi huo kwa kufungua tawi jipya na la kisasa kwenye eneo ya mradi," alisema Ulinfun.

"Tunaamini huduma hii kamili ya kibenki itasaidia kuwahudumia makandarasi, wafanyakazi na umma kwa jumla katika eneo la mradi huu. Tawi hili pia linakuja na bidhaa na huduma aina mbalimbali za kidigitali ikiwamo malipo salama na rahisi ya bili na malipo kwa njia ya mtandao ikiwa ni ishara ya benki kuendelea kuunga mkono maendeleo ya mradi pamoja na kuunga juhudi za serikali kwenye miradi mbalimbali ya ujenzi."

"Tunaiunga mkono serikali kwa sababu tunafahamu kuwa mradi huu utakuwa na mafanikio makubwa katika serikali ya Rais Dk. Magufuli ambaye amedhamiria kujenga taifa lenye viwanda vingi na mfumo bora wa uchumi na maendeleo kwa watu wake."

# Elimu ya ukatili kijinsia kupelekwa vijiweni, masoko

**Na Yasmine Protace**

ZIKIWA ni jitihada za kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia, wanaharakati wa semina za jinsia na maendeleo (GDSS), wameahidi kupeleka elimu ya ukatili wa kijinsia katika vijiwe vya bodaboda, mamalishe, babalishe na maeneo ya masoko.

Hatua ya kutoa elimu katika maeneo hayo, imechukuliwa baada ya kuona matukio ya ukatili wa kijinsia yamekuwa yakiongezeka kila uchao.

Hayo yalisemwa na Agenes Kukanga kutoka Kituo cha Taarifa na Maarifa, kilichopo Kimara, jijini Dar es Salaam.

"Kutokana na kuwapo na siku 16 za kupinga ukatili, kikundi cha taarifa na maarifa cha Kimara kimeanza kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia katika masoko, maeneo ya bodaboda, kwa kinamama lishe na baba lishe," alisema.

Ofisa Programu Idara ya Habari na Mawasiliano wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP Mtandao), Jackson Malangalila, alisema kuwa siku 16 za maadhimisho ya kupinga ukatili kaulimbiu yake ni 'tupinge ukatili wa kijinsia mabadiliko yanaanza na mimi'.

Alisema TGNP Mtandao imeanza kuwa na meendelezo wa semina za jinsia na maendeleo.

"Tumeanza mijadala na wadau wa semina za jinsia na maendeleo, uwekezaji wa rasilimali fedha, harakati za kupinga ukatili wa kijinsia," alisema.

Aliongeza kuwa katika semina hizo za jinsia na maendeleo, waliangalia huduma gani ambazo zinatolewa kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia na pia wanaharakati walizungumzia huduma zinavyotolewa.

Alisema wanaharakati waliangalia ulinzi uliopo ili masuala ya kikatili yasiendelee kutokea.

**Kutokana na kuwapo na siku 16 za kupinga ukatili, kikundi cha taarifa na maarifa cha Kimara kimeanza kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia katika masoko, maeneo ya bodaboda, kwa kinamama lishe na baba lishe**

# Jukwaa la watoto laiangukia serikali

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

JUKWAA la watoto na vijana kutoka mikoa sita nchini wanaoishi na kufanya kazi mitaani wameomba serikali kuangalia uwezekano wa kuwasaidia ili wapate haki zao kama watoto wengine, ikiwamo elimu.

Akizungumza hivi karibuni katika mkutano uliowajumuisha maofisa kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, jinsia, Wazee na Watoto, Mwenyekiti wa Jukwaa la Vijana (RCA ), Mkoa wa Mwanza, Pendo Magnusi, aliitaka jamii kuachana na mtazamo hasi juu ya kundi hilo.

Alisema jamii bado inawaona watoto hao kama wezi, vibaka ama watu wanaojiuza na hivyo kuwafanyia ukatili pasipo kutambua thamani yao.

Aliomba serikali kuwasaidia kuwakatia bima ya afya, kupata elimu ya afya uzazi, ili kuondokana na mimba zisizotarajiwa pamoja na magonjwa mbalimbali.

"Watoto wa mitaani wanakumbana na changamoto nyingi wanazofanyiwa na jamii wakiwa mitaani ikiwamo kubakwa, kufanyiwa ulawiti, kujihusisha kwenye mahusiano wakiwa na umri mdogo, hivyo tumepata fursa ya kutoa changamoto zetu tuna imani serikali itatusikia na kutupa haki zetu kwani mtoto anapokuwa mtaani hathaminiki bali anaambulia vipigo tu," alisema Magnusi.

Mwakilishi wa watoto wa mtaani kutoka Arusha, Daudi Hassan, alisema mafunzo hayo yatawasaidia kupata elimu ya afya ambayo itawasaidia kupata uelewa na kuepukana na mazingira na matendo hatarishi.

"Serikali isimamie watoto wa mitaani tupate elimu ya afya na ya kawaida ambayo itakuwa na msaada kama mimi nina malengo ya kuwa daktari au rubani japokuwa ni mtoto wa mitaani na hiyo ndoto yangu ipo siku itatimia kwa sasa nipo darasa la sita... kinachoniumiza ninapofanya biashara zangu ndogo ili nijipatie kipato watu wengine wananinyang'anya," alisema na kuongeza:

"Wakati mwingine kupigwa na walinzi wakati sisi tunahitaji haki za msingi pamoja na ulinzi, tunafanya biashara ya kuuza pipi ili nasi tujikimu."

Mkurugenzi wa Shirika la Railway Children Africa, Mussa Mgata, alisema mkakati wa shirika hilo ni kuhakikisha watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani wanaondoka na kuwa na maisha bora.

Alisema lengo la majukwaa kama hayo ni kuwapa fursa watoto waliopo katika maeneo hayo kutoa mawazo yao mbalimbali, kubadilisha uzoefu walionao kwa viongozi na wadau mbalimbali.

Naye, Ofisa Maendeleo ya Jamii Mwandamizi, Juma Samuel, aliomba mabaraza ya watoto yaliyopo nchini kuyafanyia kazi maoni ya watoto badala ya kuyapuuza.

Naye, Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Mwanza, Isaac Somba, alishukuru shirika hilo kwa kuendelea kuwapa watoto elimu ya kuwaondoa mitaani.




Mkazi wa jijini Dar es Salaam akiosha viatu vya mvua juzi, kwa ajili ya kukodishia wateja wasipate matope wanapoingia katika soko la ndizi la Mabibo kwa ajili ya kununua mahitaji. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Ukosefu hatimiliki watajwa kuwa chanzo migogoro ardhi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amewataka wananchi wilayani humo kupima maeneo yao, pamoja na kupewa hatimiliki, ili kuepuka tatizo la migogoro ya ardhi.

Alibainisha hayo juzi wakati akikabidhi hatimiliki za ardhi kwa wakazi wa Kijiji cha Jomu na Kasingili.

Alisema migogoro mingi ya ardhi ikiwamo kugombania mipaka na mashamba imekuwa ikisababishwa na wananchi kutopima maeneo yao na kupewa hatimiliki.

"Nawaomba sana, mpime maeneo yenu pamoja na kupewa hatimiliki ili kuepukana na migogoro ya ardhi," alisema Mboneko.

"Sasa hivi huduma hizi za kupewa hati miliki za ardhi, zinapatikana hapa hapa mkoani Shinyanga, hakuna tena cha kwenda mkoani Simiyu kama zamani, hivyo tumieni fursa hii vizuri kupata uhalali wa kumiliki maeneo yenu," aliongeza.

Naye Mkuu wa Idara ya Ardhi Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Julius Maira, alisema katika Kijiji cha Jomu wametoa hatimiliki 20, ambapo katika kijiji cha Kasingili wametoa hati miliki za kimila 172, na kubainisha zoezi hilo ni endelevu la kutoa hati miliki za ardhi katika vijiji vingine, ambavyo wananchi wameshalipia.

Mmoja wa wananchi waliopatiwa hati hizo, Leticia Mhoja ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Jomu, alisema hati hiyo itamsaidia kwenda kukopa fedha na kusomesha watoto wake, pamoja na kumlinda kutoporwa eneo lake ambapo kuna watu tayari walianza njama za kumnyang'anya.

# Bohora wataka Watanzania kutunza amani

**Na Moshi Lusonzo**

WAUMINI wa kiislamu wa Dawoodi Bohora nchini wameadhimisha miaka 77 ya kuzaliwa kiongozi wao duniani, Syedna Mufaddal Saifuddin, kwa kuhimiza Watanzania kutunza amani.

Akizungumza katika maadhimisho hayo yaliyoambatana na maandamano yaliyoishia katika Msikiti Mkuu jijini Dar es Salaam, Sheikh Saifuddin Jamal, alisema amani ya nchi ni nguzo katika kuwajengea watu umoja na upendo.

Alisema maadhimisho hayo ya kiongozi wa kiroho inawakumbusha kila muumini kuishi kwa kufuata sheria na kuepuka vitendo vitakavyomchukiza Mungu na jamii inayowazunguka.

"Sisi waumini katika kipindi hiki tunahimiza upendo na amani kwa kila mtu, hata kiongozi wetu Saydna Mufadal tutangaze kwa vitendo jambo hilo," alisema Jamal.

Alisema kwa kuishi maisha hayo ya unyenyekevu ni sawa kuwa pamoja na mtume Muhammad SAW, ambaye alisema mapenzi ya nchi ni sehemu ya utukufu.

Akizungumza kazi walizofanya katika maadhimisho hayo ni pamoja na kutoa misaada mbalimbali kwa watoto yatima Kijiji cha Vianzi mkoani Pwani.

Alisema waumini wa Dawoodi Bohora, wamesambaa katika nchi zaidi ya 40 ambao husaidia katika masuala mbalimbali ya kijamii ikiwamo elimu, afya, utunzaji mazingira, usawa wa kijamii na utoaji misaada sehemu zenye matatizo ya ukosefu wa chakula.

Katika maadhimisho hayo, waumini wanapata muda wa kutafakari kwa matendo mema ya kiongozi wao, kutoa hutuba na kuendesha michezo mbalimbali.

# Wanaodaiwa nyumba zao kuchomwa na askari TAWA waiangukia serikali

**Na Gurian Adolf,** NKASI

BAADHI ya wananchi ambao nyumba zao zilichomwa moto na askari wa TAWA waliopo katika pori la akiba la Lwafi wilayani Nkasi mkoani Rukwa, wameomba serikali iwasaidie.

Wanadai kuwa wanakabiliwa na changamoto mbalimbali katika msimu huu wa mvua za masika zinazonyesha wilayani humo.

Wakizungumza na gazeti hili, walisema kuwa askari hao wa TAWA walichoma nyumba zipatazo 150 katika kijiji cha Itete wilayani Nkasi kwa madai kuwa nyumba hizo zimejengwa ndani ya Pori la Akiba la Lwafi.

Mwenyekiti wa serikali ya kijiji hicho, alisema kuwa familia zilizokuwa zikiishi katika nyumba hizo zimebaki bila makazi kutokana na kitendo hicho, hivyo wanahitaji misaada kutoka serikali ama kwa taasisi mbalimbali.

Alisema baadhi yao wana watoto, hivyo wanaishi katika usumbufu mkubwa licha ya kuwa Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini, Aida Khenan ambaye ni mbunge wa jimbo hilo, ametoa msaada wa maturubai 100 ili wayatumie kujikinga na mvua zinazoendelea kunyesha.

Hata hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Said Mtanda, alimwagiza ofisa ardhi wa wilaya Nkasi kulipima upya eneo lote la pori hilo la akiba kwa kutumia GPS na kujenga alama ya mipaka ya kudumu na si kuweka vibao ambavyo vimekuwa vikihamishwa mara kwa mara na kusababisha changamoto hizo.

Alisema umefika wakati ni lazima tatizo la mipaka kati ya wananchi na hifadhi za wanyamapori likomeshwe wilayani humo kwani limekuwa likisababisha usumbufu mkubwa kila mwaka, na kuwasababishia hasara kubwa na usumbufu wananchi wanaoishi kwenye vijiji vinavyopakana na hifadhi hizo.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, akijaza mafuta kwenye gari ya mteja wakati akizindua Wiki ya Mteja 2020 ya kampuni ya Puma Energy Tanzania Ltd, katika kituo cha Upanga, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Puma Energy, Dominic Dhanah. **PICHA: JOHN BADI.**

# Sababu uwapo wajiolojia feki zaanikwa

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

WIZARA ya Madini imesema Watanzania walichelewa kujua chanzo cha jiolojia na madini, hivyo kusababisha kuwapo kwa wajiolojia feki wanaotengeneza ripoti za utafiti wa madini.

Akizungumza juzi wakati wa kufunga mkutano mkuu wa mwaka wa Jumuiya ya Wajiolojia Tanzania (TGS) uliofanyika jijini Mwanza, Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Profesa Saimon Msanjila, alisema kuwa Tanzania ina rasilimali nyingi yakiwamo madini ya aina mbalimbali.

"Watanzania tulichelewa kujua chanzo cha jiolojia na madini, ndiyo maana tumeibiwa sana, hali hiyo imesababisha kuwapo wajiolojia feki wanaotengenza ripoti za utafiti wa madini...sasa dawa yao ni kuanzisha baraza la wajiolojia litakalokuwa likisimamia," alisema.

Profesa Masanjila alisema kuwa Tanzania ina raslimali za madini ya aina mbalimbali yakiwamo ya shaba, almasi, rubi, nikel, tanzanite, ambayo hayapatikani kwingineko dunia, miamba ya mawe, makaa ya mawe, gesi pamoja na madini mengine ambayo hayajawahi kuchimbwa tangu yagunduliwe.

Aidha, alisema kuwa utendaji mzuri wa kazi katika sekta hiyo utasaidia kuwaondoa vishoka wa madini, huku akiwataka wananchi, wadau na wachimbaji wadogo na wakubwa kutumia uzalendo ili kutimiza wajibu wao badala ya kuhujumu uchumi wa nchi yao.

Katibu Mkuu huyo alisema kuwa kuwapo kwa wataalamu wa jiolojia na madini kumechangia uchumi wa taifa kuongezeka mara dufu, ikiwamo uendeshaji wa viwanda na utoaji wa ajira kwa Watanzania.

Hata hivyo, alisema kuwa katika sekta ya madini bado kuna changamoto kubwa kwenye soko lake, hivyo serikali ina wajibu wa kuimarisha soko hilo, ili wachimbaji wadogo na wakubwa waweze kuneemeka.

Alisema kuwa sekta ya madini hivi sasa inasifiwa nchini katika kuongeza pato la taifa, lakini bado haijafikia kiwango kinachotakiwa cha uzalishaji.

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 1, 2020
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 12
**Kupandikiza uroto kunaweza kuwa tiba VVU**



Ukurasa 14
WARAKA KWA SERIKALI



Ukurasa 13
**Udhibiti mimba shuleni 'unasahauje' uchunguzi wa maambukizi ya VVU?**

ELIMU

# DAUDI MWIGAMBA

- Ana kipaji cha kipekee, hujibu kila swali 'fasta'
- Anajua wakuu, mataifa, miji mikuu duniani

NA MWANDISHI WETU

DAUDI Mwigamba, kwa kutumia lugha za mitaani anaweza kuelezewa kuwa ni 'kichwa' kutokana na kipaji cha kipekee alicho nacho. Ana uwezo wa kukamata mambo na kuyaweka kichwani kwa muda mfupi bila kuyasahau.

Hata kama akishtuka kutoka usingizini, ameziweka taarifa zote za dunia kiganjani mwake. Na unapomuuliza swali kuhusu majina ya mataifa, miji mikuu, marais, viongozi wengine kama makamu rais na uwaziri mkuu, anakujibu bila kukosea.

Hii inamaanisha kuwa Daudi ni kitabu cha ramani au 'Atlas' inayoishi. Nipashe inapokutana naye shuleni kwake Tusiime Sekondari Dar es Salaam, anadhihirisha umahiri huo kwa kutaka aulizwe swali lolote kuhusu Jografia, likihusu rais, mji mkuu na maelezo mengine muulizaji atakayo. Na swali likawa hivi.

"Taja jina la rais wa kisiwa cha Sao Tome and Principe, mjini mkuu na mahali kilipo":

Anajibu: Rais ni Manuel Pinto da Costa, jiji kuu ni Sao Tome na kisiwa kipo jirani na Equatorial Guinea. Pengine ni wanafunzi wangapi wa Jiografia kuanzia shule za sekondari hadi vyuo vikuu na watu wengine wanaojua kisiwa hicho? Kwa Daudi ni jambo jepesi.

### HISTORIA YA KIPAJI

Anasema, hana haja ya kutumia 'Atlas' dunia yote iko kichwani. Pia majina ya viongozi wake, miji na matukio yanayoendelea kwenye mataifa hayo.

Anasema amekuwa na umahiri wa kusoma mambo mengi na kuyaweka kichwani hasa ya Jiografia tangu akiwa mdogo na kwamba mama yake ndiye aliyempa moyo wa kuendeleza kipaji hicho.

"Nilikuwa napenda sana somo hilo na mama alinunua Atlas za kila aina. Nasoma na kufuatilia taarifa zake kujua zaidi, na huo ukiwa mwanzo. Nilikuwa na miaka 10 niko darasa la nne nilitumia wiki moja kuiweka Afrika yote kichwani. Nikawa najua kila taifa, mji mkuu, jina la rais au kiongozi wake na mahali lilipo."

Anasema mwanafunzi huyo ambaye familia yake inatokea Ukerewe - Mwanza.

"Nilipoona nimeifahamu Afrika ilinichukua kama wiki mbili kuweka kichwani ramani ya dunia. Nikujua kila taifa, mji wake mkuu na rais bila kutetereka," anasema kijana huyo mwenye miaka 19.

Daudi yuko kidato cha sita mchepuo wa sayansi - Fizikia, Kemia na Hisabati (PCM), akilenga kuwa kinara wa masuala ya kielektroniki kwenye teknolojia ya mawasiliano (IT).

"Kuanzia mwaka 2015 nyakati za mahafali nilikuwa nazungumza na kuhamasisha ufahamu wa masuala mbalimbali nikitumia muda huo kutaja nchi, kiongozi na mji mkuu. Sasa nabadilisha nimeelekea kwenye mawaziri wakuu na makamu rais," anasema.

Anaeleza kuwa wakati wote, anaangalia kwenye mitandao kujua iwapo kuna mabadiliko ya kiongozi duniani ili kujiweka sawa kwenye eneo hilo na kuendelea kuwa 'Atlas inayopumua' .



Mwigamba akishika kipaza sauti kufanikisha mwanafunzi mwenzake kufikisha ujumbe kwenye moja ya majukwaa ya kielimu shuleni kwao. **PICHA: TUSIIME**

### UJASIRI NA UONGOZI

Daudi anasema licha ya kuzaliwa na hali ya ualbino, amejikubali na anafanya kila jambo bila hofu au kujiuliza wengine watawaza nini kuhusu yeye.

Anasema ni rais mstaafu wa serikali ya wanafunzi wa Tusiime. Amefanyakazi hiyo kuanzia mwaka 2019 hadi mwaka huu nilipoingia kadato cha sita na kwamba amejituma kwenye uongozi na ana mengi ya kujivunia.

Anaeleza kuwa licha ya viongozi wa shule hiyo kumpenda na 'kupigia debe' kuwa anafaa kusikiliza na kutatua shida za wengine, hivyo apewe jukumu hilo la kiongozi mkuu wa shule, anafurahi maana wakati wa kupiga kura wanafunzi wenzake walimpigia nyingi.

Anakumbusha kuwa alizoa zaidi ya kura 900 kati ya takribani 1,000 zilizopigwa, jambo lililomtia moyo kuwa anakubalika.

### HALI KIMASOMO

Daudi akizungumzia masomo anasema anapambana na changamoto za uoni hafifu kwa kutumia vifaa saidizi kuongeza uoni, anasema walimu wake wanafahamu na kumsaidia kila anapohitaji msaada.

Akiwa darasani anakaa eneo ambalo anaona ubaoni, kumsikia mwalimu na anatumia miwani na kikuza maandishi kiitwacho 'monocular' na kwamba familia yake hasa mama yake amekuwa msaada na ndiye anayempatia vifaa saidizi.

### UJUMBE MUHIMU

Daudi anasema wiki hii dunia inapoadhimisha Siku ya Wenye Ulemavu, anawataka wenye ualbino kujikubali na kujua kuwa mwenye ualbino hana tofauti na binadamu wengine, wanafafana kwa kila hali na tofauti ni rangi.

"Wenye ualbino wamekosa au wana upungufu kwenye rangi ya asili kwenye ngozi, nywele au machoni. Lakini, hawana tofauti na binadamu wengine. Wote tunafikiria, tunahisi njaa, tuna akili na vipaji, tuna hisia zote ni binadamu tuliokamilika." Anasisitiza.

Aidha, anawakumbusha wazazi kuwa mtoto anapozaliwa na hali ya ualbino wasianze kutafuta sababu au kuwa na hisia za kufikirika ambazo hazina ukweli na kuwachukia watoto wao.

"Inafaa na ni muhimu kujikubali, kujichanganya, kuongea na kuchangamka na kuacha kujinyanyapaa kwa vile kama walivyo wengine, ndivyo walivyo wenye ualbino wote ni binadamu wa kawaida.

Anawataka wenye ualbino shuleni na popote walipo washirikiane na wenzao kama kuna kitabu wanahitaji kusoma, lakini hawawezi au hakuna chenye maandishi makubwa, wawaambie wenzio wawasomee na wajitahidi kimasomo ili wasibaki nyuma.

Anawataka wasiogope na kujirudishe nyuma kwa sababu elimu inatolewa bure na huo ndiyo wakati wa kutumia fursa na kujiendeleza, wakiwa darasani waombe msaada wanapouhitaji, huku wakichana na hisia za kujikataa na kuwa wanyonge.

"Ukianza kujinyanyapaa familia na jamii itafanya hivyo pia. changamka, jichanganye na kujiamini. Mwenye ualbino ni binadamu wa kawaida ana uwezo kama wengine, hivyo ni lazima kujishughulisha."

Mwalimu Mkuu wa Tusiime Sekondari, Emilius Rugambwa, akizungumza kipaji cha Daudi, anasema pomoja na uwezo huo mkubwa wa darasani na nje ya shule, ana kipawa cha umahiri wa kuzungumza na kuamsha hisia (motivational speaker).

ELIMU

**NA MWANDISHI WETU**

# Kupandikiza uroto kunaweza kuwa tiba VVU

## • Mwathirika aliyebadilishiwa aishi bila ARV

MWISHONI mwa 1970 dunia ilishuhudia ujio wa maradhi ya Ukimwi na tangu wakati huo watafiti hawajaacha kusaka dawa kwa ajili ya kukabiliana na virusi vinavyoharibu na kudhoofisha mfumo wa kinga mwilini na kusababisha maradhi mengi yasiyo na tiba.

Miongo minne ya kusaka tiba na chanjo haijawa na mafanikio sana kwa vile dawa zinazotumiwa ni za kudhoofisha VVU mwilini lakini si za kuviua.

Miaka ya karibuni jitihada za kutibu VVU zimeendela kutia moyo baada ya mgonwja wa pili aliyebadilishiwa uroto (bone marrow) kuendelea kuishi bila kuwa na virusi vya Ukimwi mwilini.

Mgonjwa huyo aliyetibiwa kwa kuwekewa uroto mpya ni Adam Castillejo, ambaye hadi sasa anaendelea kuishi na kubandikwa jina la "London patient", au mgonjwa wa London ni mzima hata baada ya miezi 18 (mwaka 1.5) wa kuacha kutumia dawa za kudhibiti makali ya VVU (ARVs) .

Mwaka huu 2020 wataalamu wa afya walipomwondolea dawa za ARV miaka miwili (miezi 46) baada ya kumpa uroto mpya, Castillejo aliendelea kuwa salama na kwamba wataalamu wanajitahidi kuchunguza uwepo wa VVU kwenye maeneo mbalimbali ya mwili wake lakini hawakuona virusi hivyo.

"Havikuonekana virusi kwenye damu, maji ya uti wa mgongo, njia ya chakula, manii wala kwenye matezi ya mitoki," linasema gazeti la The Guardian London.

Linaongeza kuwa ripoti hiyo inaeleza kuwa kubadilisha uroto kunaweza kuwa tiba ya VVU na Ukimwi licha ya kwamba kuna kazi kubwa zaidi.

Timu ya watafiti ilisema kuwa iliona baadhi ya mabaki ya VVU kwenye seli, lakini ni mfu zikiwa kwenye nasaba (DNA) kwenye baadhi ya seli nyeupe (white cells), na hazikuwa na uwezo wa kuzalisha virusi tena ni kwa mujibu wa Prof. Ravindra Gupta, wa Chuo Kikuu cha Cambridge, aliyekuwa mtafiti wa kwanza wa eneo hilo.

Castillejo mwenye miaka 40 kwa mara ya kwanza alihojiwa na vyombo vya habari na kueleza kuwa ameishi na HIV tangu mwaka 2003.



Adam Castillejo, mwathirika aliyebadilishiwa uroto, ameendelea kuishi kwa zaidi ya mwaka sasa akiwa hana VVU kwenye damu. **PICHA: MTANDAO**

> Havikuonekana virusi kwenye damu, maji ya uti wa mgongo, njia ya chakula, manii wala kwenye matezi ya mitoki.



Kupandikaza uroto ndani ya mifupa ya damu, kunaweza kufanikisha tiba ya VVU badala ya ARV ambazo inadaiwa haivimalizi virusi bali kuvidhibiti. **PICHA: MTANDAO**

### HISTORIA YA TIBA

Mwathirika Castillejo anakuwa mtu wa pili mwenye Ukimwi aliyeondolewa virusi hivyo kwa kubadilisha viwanda vya 'kuzalisha damu,' au 'bone marrow.'

Mapema mwaka jana jopo la wanasayansi lilitangaza kufanikiwa kumwondolea virusi mwathirika wa VVU kwa kutumia tiba ya kumpandikiza uroto kutoka kwa mtu ambaye hajaathirika na virusi hivyo.

Tiba hiyo ilioonyesha mafanikio baada ya majaribio ya mwanzo ya mwaka 2007.

### KINACHOFANYIKA

Madaktari wanatumia njia ya kupandikiza uroto ndani ya mifupa ili kumpa seli mpya za kuzalisha damu isiyoathirika ili kuviondoa virusi vya Ukimwi kwa mwathirika.

Ingawa wanasifu matokeo ya utafiti huo, lakini wanaonya kwamba ni mapema mno kumthibitishia kwamba amepona.

Wanasema Castillejo aliyekuwa ameambukizwa VVU yuko katika hali nzuri.

Akiwa amepachikwa jina la "mgonjwa wa London," ameondolewa virusi hivyo vilivyoathiri takriban watu milioni 37 duniani kote.

Wanasayansi walitumia njia ile ile ambayo ilitumiwa na kuonyesha mafanikio kwa mgonjwa wa VVU mjini Berlin, hapa Ujerumani mwaka 2007.

Kiongozi wa jopo la utafiti huo, Ravindra Gupta, alinukuliwa akisema "Kufikiwa kwa hatua hii kunakoonyesha ahueni kwa mgonjwa huyu wa pili na kulikotokana na mbinu ileile iliyotumiwa awali kwa mgonjwa wa kwanza wa Berlin.

Katika visa vyote viwili, wagonjwa walipandikizwa uroto kutoka kwa watu waliokuwa na uwezo wa kuhimili VVU. Lakini alisema, kubadilisha chembe hai za mwathirika na watu hao kumeonekana kumwezesha mgonjwa kuzuia VVU vya Ukimwi kurejea baada ya matibabu.

Kwa mujibu wa Gupta, mgonjwa wa London aligunduliwa na VVU mwaka 2003 na amekuwa katika tiba ya kudhoofisha makali ya VVU tangu mwaka 2012, ARV. Tiba hiyo hudhoofisha virusi hivyo na si kuviondoa. Alifanikiwa kupandikizwa uroto 2016, lakini akiendelea kutumia tiba kwa muda wa miezi 16 kabla ya kuacha matibabu hayo.

Na tangu hapo, hajaonyesha dalili yoyote za kuwa na virusi kwa miezi 19 sasa. Profesa Gupta anasema hawajaona virusi hata baada ya kumpima. Hata hivyo, alionya kwamba "ni mapema mno kusema kwamba amepona."

Mtafiti huyo alisema mafanikio haya ya mara ya pili ya kuviondoa VVU kwa kupandikiza uroto yatasaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa utafiti wa kimatibabu kwa miaka inayokuja.

### TAHADHARI

Profesa Gupta anaonya kuwa upandikizaji huo wa uroto ni hatari, unaouma na unatumia gharama kubwa, hivyo hauwezi kuwa chaguo bora zaidi la matibabu ya VVU.

Alisema ni asilimia 59 pekee ya watu wanaoishi na VVU duniani kote wanapata ARV. Aidha, takribani waathirika 1,000,000 hufa kila mwaka kutokana na magonjwa yanayohusiana na VVU na Ukimwi.

Kadhalika, karibu watu milioni 35 wamekufa kutokana na Ukimwi tangu kuanza miaka ya 1980.

**DW / The Guardian London**

ELIMU
NA SABATO
KASIKA
SIKU YA UKIMWI DUNIANI

# Udhibiti mimba shuleni usisahau uchunguzi maambukizi ya VVU

NI kilele cha Siku ya Ukimwi Duniani, wakati ambao takwimu zinaonyesha kuwa Watanzania takribani 100,000 huambukizwa VVU kila mwaka.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Uwekezaji, Dorothy Mwaluko, anayasema hayo wakati akizungumza na wanahabari jijini Dodoma, hivi karibuni, kuhusu maadhimisho ya Siku ya Ukimwi.

Anasema, takwimu zinaonyesha kuwa, takribani watu 72,000 wanapata maambukizi mapya kwa mwaka na kwamba hiyo inamaanisha kuwa kwa mwezi ni watu 6,000.

"Kwa hesabu hizo kwa siku watu 200 wanaoambukizwa na kwa saa moja ni watu wanane, hivyo mikakati madhubuti inahitaji."

Siku ya Ukimwi Duniani, huadhimishwa Desemba mosi kila mwaka baada ya Umoja wa Mataifa, kutenge siku hiyo kwa lengo la kuongeza juhudi zaidi kuudhibiti.

Mwaluko anasema zaidi ya asilimia 50 ya maambukizi mapya ya VVU nchini yako kwa vijana wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 35.



Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**MIKAKATI KUDHIBITI**

Akizungumzia mbinu na mikakati ya kudhibiti, Mwaluko anasema ni ya namna mbili ili kukabiliana na hali hiyo.

Anataja mkakati wa kwanza kuwa ni kwa kundi lililoambukizwa kufubaza virusi na kuendelea kufanya kazi, kwa kuwa mtaji wa maskini ni nguvu na sio virusi.

Wa pili ni kuweka mikakati ya kuwalinda wale wasioambukizwa wasipate VVU.

Anasema, ili vijana wasiambukizwe, ni muhimu waongozwe, watambue kuwa miili yao ndiyo maisha yao na pia maisha yao ndiyo nguvu ya ujenzi wa taifa lao, hivyo ni vyema waepuke njia zinazowapeleka kupata Ukimwi.

**UKIMWI NA MIMBA**

Kundi linaloambukizwa zaidi ni vijana, ambao baadhi yao ni wanafunzi, ambayo ndiyo nguzo ya taifa, wanaopaswa kuelimishwa ili kuepuka maradhi hayo, kwa mujibu wa maelezo yake.

Wanawake ndiyo wanaopata mimba ambazo zinaweza kusababisha VVU, kwa kuwa njia kuu ya maambukizi ni kujamiiana.

Kumekuwapo na taarifa kutoka maeneo mbalimbali za mabinti wa shule za msingi na sekondari kukatisha masomo kwa sababu ya mimba.

Haitoshi kuishia kwenye mimba, suala la VVU linastahili kipaumbele kwa vile anayepewa ujauzito inawezekana ameambukizwa VVU.

Pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau wa elimu na afya kudhibiti tatizo hilo, mimba zimeendelea kuripotiwa kutoka mikoa mbalimbali.

Kuendelea kuwapo mimba shuleni kunaashiria uwezekano wa maambukizi ya VVU, hivyo elimu ya afya ya uzazi ni muhimu kuepusha hatari hiyo.

Mathalani, ndani ya miezi tisa, wanafunzi 151 wa msingi na sekondari mkoa wa Lindi wamekutwa na mimba, lakini hakuna taarifa za maambukizi ya VVU.

Kama taarifa hizo ni kwa Lindi pekee vipi nchi nzima wako wanafunzi wangapi wenye ujauzito wanaweza kuwa na maambukizi?

**MWONGOZO SHULENI**

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli, anasema serikali inakamilisha mwongozo wa kuimarisha elimu kuwezesha mwanafunzi kuepuka mimba.

Anasema mwongozo ukikamilika serikali itatoa mafunzo maalumu kwa walimu watakaowapa elimu ya kukwepa vishawishi mabinti wanaopevuka shuleni.

"Tumepanga kuanza na walimu wawili kila shule ili watoe elimu jinsi ya kuepuka vishwawishi na kujilinda wasipate mimba za utotoni na kukatishwa masomo yao," anasema Mweli

Kwa mujibu wa Katibu programu inalenga kupunguza mimba za utotoni na zisizotarajiwa ili wasichana wanapoanza shule wanamalize.

Mweli anataja mkakati mwingine kuwa ni ujenzi wa mabweni na kwamba hadi sasa asilimia 90 ya yaliyojengwa ni ya wanafunzi wa kike na kwamba, serikali inataka mtoto wa kike awe salama, hasa kwenye maeneo ambayo wanatembea umbali mrefu.

"Tunalenga kuwa ifikapo mwaka 2025 maeneo ambayo ni hatarishi, wanafunzi wanapata mabweni na kuishi shuleni, tunataka mwanafunzi asipate mimba," anasema.

**HALI KIMATAIFA**

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kushughulikia Ukimwi (UNAIDS), linakadiria kuwapo takribani vijana 6,000 wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24 duniani, wanaopata UVV kila wiki.

> "Tumepanga kuanza na walimu wawili kila shule ili watoe elimu jinsi ya kuepuka vishawishi na kujilinda wasipate mimba za utotoni na kukatishwa masomo yao.

Shirika hilo linashauri kuwekeza katika elimu ya afya ya uzazi ili kupunguza na hatimaye kutokomeza ugonjwa huo.

Aidha, likuzungumzia matibabu ya VVU, UNAIDS inasema yameongezeka na hadi kufikia katikati mwa mwaka jana, kulikuwa na zaidi ya watu milioni 24 waliokuwa wanaishi na VVU na wakitibiwa wakiwamo vijana wanawake milioni 13 wenye umri wa miaka 15.

Ripoti ya shirika hilo ya mwaka huu, inaeleza kuwa kuna hatua mbalimbali za mafanikio kwenye vita dhidi ya maradhi hayo japo zinahitajika juhudi zaidi.

Mkurugenzi Mtendaji wa UNAIDS Winnie Byanyima, anasema shirika linaangazia ukosefu wa usawa na haki kwenye janga la VVU linavyowakabili wanawake na jinsi mapungufu katika haki na huduma, vinavyozidisha tatizo.

Ripoti hiyo ya UNAIDS inasema, kuna mafanikio katika maeneo ya msingi, kutokana na kwamba wasichana wengi wako shule na pengo la jinsia katika shule za msingi linapungua duniani kote.

ELIMU

**NA GAUDENSIA MNGUMI**



Wanafunzi wenye ualbino wanaomba 'mkono wa serikali' kupata vifaa visaidizi darasani kukabili uoni hafifu, mafuta na miwani kuwaepusha na athari za jua. **PICHA: MTANDAO**

# WARAKA KWA SERIKALI

- Inavyohudumia VVU iwafikie wenye ualbino
- SOSPA ibadilike, anayebaka wenye ulemavu jela miaka 40

NILIHUZUNIKA siku nilipokwenda kwenye hospitali inayohudumia watu wenye mahitaji maalumu nikakutana na mzazi aliyenikatisha tamaa kwa namna alivyokosa upendo na kumthamini mwanawe. Kwa mshangao, nikiwa na dada pamoja na mama yangu tulihamaki, alipouliza, hivi watoto hawa wenye ualbino wanaweza kusoma?"

"Ni swali alilouliza mzazi wa mtoto wa miaka saba, mwenye ualbino ambaye anashangaa kuona kuwa tunasoma, niliumia."

Ni maneno ya Hamad Jumbe, mwanafunzi wa kidato cha tano anayesomea ECA katika Shule ya Tusiime Dar es Salaam, anapozungumza na Nipashe kuhusu siku ya wenye ulemavu duniani, inayoadhimishwa kila mwaka Desemba 3 na mahojiano yakilenga maisha ya wanafunzi na watoto wanaoishi na ualbino.

Hamad anasema mzazi huyo kutoka Morogoro alimleta mtoto wake hospitalini CCBRT Dar es Salaam, ni kielelezo kuwa wazazi, walezi na jamii inahitajika kufahamishwa kuhusu hali ya ualbino na ziwe jitihada endelevu.

Anasema yeye na dada yake wana hali ya ualbino na mama yao aliwapeleka hospitalini kuchunguzwa macho, ili kutibu uoni hafifu na katika maongezi yao, mzazi huyo akashangaa kusikia kuwa wanasoma.

"Mama alimfahamisha kuwa tunasoma na kwamba mtoto wake anastahili kutibiwa na pia amechelewa kusoma hivyo, aharakishe kumsajili aanze shule".

> Kila wakati ilikuwa zogo, Hamad unatuziba, Hamad toka huku nikisukumwa... yote hayo ni kwa sababu wenzangu walikuwa hawafahamu tatizo la uoni hafifu nililonalo.

Hamad anahisi wazazi na walezi wanaweza kuwa kikwazo kwa maendeleo ya wenye ualbino hivyo wakati umefika kuwaelimisha na kuwafahamisha kuwa hakuna kilichopungua kwa wenye ualbino ni watu wa kawaida, licha ya kuwa na uhaba au kukosa rangi ya kawaida kwenye ngozi, macho na nywele.

"Hata walimu nao wapewe elimu kuwajali na kuwapa nafasi wenye ualbino ili watusaidie na tutimize malengo yetu kielimu." Anasisitiza Hamad Jumbe ambaye baba yake ni mzaliwa wa Tanga na mama Kigoma.

**ALIPOTOKA**

Hamad anasema mwanzo wake shuleni ulikuwa mgumu, kwa vile alikuwa na uoni hafifu tangu mwanzo na ilikuwa changamoto kusoma ubaoni.

"Nilikuwa na uoni hafifu. Mama alijua tatizo langu na kupeleka taarifa shuleni. Lakini, pamoja na jitihada hizo kama walivyo wazazi wengine hakufahamu kuwa ukiwa na hali ya ualbino mara nyingi unakosa rangi ya asili kwenye macho kwa hiyo mwanga unakuumiza, huoni unatakiwa uanze kuvaa miwani mapema," anakumbusha Hamad.

Shuleni, anasema alisumbuka mno kuona na kuandika 'notes' ubaoni. Alilazimika kuzunguka na kukaa kila eneo alilohisi anaona vizuri na kuanza kunakili.

"Kila wakati ilikuwa zogo, Hamad unatuziba, Hamad toka huku nikisukumwa... yote hayo ni kwa sababu wenzangu walikuwa hawafahamu tatizo la uoni hafifu nililonalo." Anasema mwanafunzi huyo ambaye ni mnyenyekevu na mtaratibu, anayejiamini na kujithamini.

Anaeleza kuwa mama yake alikuwa anafuatilia masomo shuleni na kumuuliza anayokutana nayo, alimwelezea kuhusu tatizo la kuona ubaoni na mzazi wake akalipeleka kwa mwalimu mkuu, aliyewaeleza walimu wengine kuhusu Hamad kukaa mbele, ili asikie na kukuza herufi ili kumwezesha kuziona.

"Kuna wengine walilipokea vyema na wapo waliopuuza. Walimu wengi wakawa wananiita Hamad sogea mbele. Unaona vizuri? Ikafika wakati na wenzangu darasani wakawa wanawakumbusha walimu ...Mwalimu Hamad asogee, akae mbele," anasema yote hayo yalimtia moyo.

**UPENDO NI KILA KITU**

Anakumbusha kuwa wenye ualbino wanahitaji upendo, kushirikishwa na kusaidiwa popote walipo. Anasema jamii yake hasa marafiki na majirani huko Mbagala alipokulia na Shule ya Yemens alikosoma walimpa yote hayo.

"Lakini bado msimamo wangu ni kwamba walimu wanahitaji kupewa elimu ya ualbino. Siku hizi sera ni elimu jumuishi serikali ihakikishe wanafahamishwa kuhusu ualbino popote walipo iwe mijini au vijijini," anasema na kushauri wafahamishwe kwenye semina au mikutano ya kikazi.

**KUTIBU WENYE UALBINO**

Hamad Jumbe, anayesoma mchepuo wa uchumi, biashara na uhasibu (ECA) anasema kila mara kuna kampeni zinazolenga wenye VVU ili kuokoa maisha yao akitaja ile ya 'FURAHA YANGU'.

"Kama ambavyo wanahimizwa kila mara kupima, kujua hali na kuanza dawa na kuzitumia kwa usahihi ili waishi kwa furaha, vivyo hivyo wenye ualbino nao wasaidiwe."

Serikali iwafikie, wapimwe afya hasa ngozi na macho. Wapewe mafuta na tiba za kusaidia tatizo la ngozi, kulinda maisha kama inavyofanyika kwa wanaoishi na VVU, ili kuwaepusha na saratani.

"Tunaiomba serikali itenge bajeti kwa ajili wenye ualbino kwenye elimu na matibabu hasa familia maskini vijini na mijini. Kama inavyofanyika kwa wenye VVU." Anaomba.

Anasema wanaoishi katika familia masikini wanahitaji vifaa saidizi kwenye uoni hafifu, miwani, vitabu vyenye maandishi makubwa, lenzi, tiba ya ngozi, mafuta ya kukinga athari za mionzi hatarishi na mavazi.

**ULINZI KISHERIA**

Hamad anasema wanaoishi na ulemavu wapo kwenye mazingira hatarishi kwa mfano, mabinti wanakabiliwa na umaskini, kubakwa, mimba za utotoni na unyanyasaji.

Anashauri kuwa ili kulinda haki, utu na heshima ya binti anayeishi na ualbino na ulemavu wowote, sheria ya makosa ya kujamiiana (SOSPA) ifanyiwe tena marekebisho na washtakiwa wafungwe miaka 40.

Tunahitaji pia Wizara ya Sheria na Katiba, Afya na Ofisi ya Rais-Serikali za Mitaa ziandae sheria ya kukomesha wanaume kuwatelekeza wake zao pale wanapojifungua mtoto mwenye ualbino. Kuwe na sheria mahususi kukomesha na kutoa adhabu kali kwa wanaotelekeza mtoto anayezaliwa na ualbino au ulemavu mwingine.

Anashauri hayo kwa sababu baadhi ya wanaume na ndugu zao huwafukuza na kuwatuhumu wanawake wanapopata watoto wenye hali hiyo.

"Jamii inawachukulia kuwa ni laana, mikosi wakati ni maumbele. Tena wanazaliwa na wazazi wote wawili, kwa sababu utafiti umethibitisha kuwa ili kupata mtoto mwenye ualbino ni lazima baba na mamawe wawe na nasaba zenye ualbino. Sasa kwanini mama anyanyaswe? Inahitajika elimu na sheria zinazokomesha udhalimu," anashauri.



## Tunu Pinda ataka riba nafuu mikopo kwa wajasiriamali

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKE wa Waziri Mkuu mstaafu, Tunu Pinda, ameiomba serikali kuanzisha taasisi za kibenki zitakazowawezesha wajasiriamali kwa kuwakopesha mikopo ya riba nafuu kwa ajili ya kuongeza mitaji yao.

Mama Pinda alisema hayo alipokuwa akifungua mafunzo ya ujasiriamali kwa ajili ya kinamama yaliyofanyika jijini Dodoma.

Alisema serikali ikianzisha taasisi hizo za kibenki ambazo zitakuwa zikitoa mikopo yake kwa riba nafuu, itawaondolea unyanyasanji na dhuluma wanayofanyiwa mitaani na watu ambao wamekuwa wakitoza riba.

Alisema taasisi za kibenki zinazokopesha mitaani zimekuwa zikiwadhulumu na kuwanyanyasa wajasiriamali wanawake wanaokopa mikopo na kushindwa kulipa kwa wakati, hivyo aliiomba serikali kuliangalia sula hilo ili kutafuta namna ya kuwakomboa kinamama pamoja na watu wengine.

"Taasisi hizo za mitaani kwa kweli zimekuwa zikiletea umaskini kinamama, wengi kwa kunyanganywa mali zao kutokana na tozo kubwa ya riba wanayotakiwa kutoa, hivyo tunaiomba serikali yetu sikivu kuliangalia hili kwa mapana zaidi ili kuwakomboa kinamama hao wanaojishughulisha kwa ajili ya maendeleo yao na nchi kwa ujumla," alisema.

Hata hivyo, aliwataka wanawake wanaokopa fedha hizo kutoka taasisi za kifedha kuwa waangalifu kwenye matumizi yao, ili kumudu kulipa mikopo wanayokopa, na kuwa kwa kufanya hivyo itawaondolea manyanyaso.

"Matatizo mengine tunajitakia wenyewe tu, ukipata fedha hizo kinachofikiriwa ni kujipamba kwa gharama kubwa na kujiingiza kwenye starehe ambazo hazina faida,wakati fedha hizo siyo malengo yake yaliyokusudiwa ya kujiinua kiuchumi na kukuza mitaji yao," alisema.

Mratibu wa mafunzo hayo, Mchungaji Yamnyausi Mwaluko, alisema lengo la mafunzo hayao ni kuwafanya wajasiriamali wanawake kufanya shughuli kwa malengo ya kuufikia uchumi wa kati pamoja na maendeleo yao.

# Wanafunzi watakiwa kuwafichua wanaochoma mabweni, madarasa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WANAFUNZI wa shule za sekondari na msingi, wametakiwa kutoa ushirikiano kwa serikali kuwafichua watu wanaojihusisha na vitendo vya uhalifu vya uchomaji mabweni na madarasa.

Rai hiyo ilitolewa na wanafunzi wanaosoma shule za sekondari mkoani Dodoma, walipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Michael Kusenah, mwanafunzi wa Shule ya Dodoma Sekodari kidato cha tatu, alisema wanafunzi wakitoa ushirikiano, serikali itafanikiwa kuwabaini watu wote wanaohujumu na kuharibu miundombinu ya shule.

Alisema wanafunzi wana mchango mkubwa wa kufanikisha kukamatwa kwa watu hao ambao wengi wao ni kutoka katika jamii zao.

"Hivyo ninawaomba wanafunzi wenzangu kote nchini tutoe ushirikiano kwa serikali yetu kuhakikisha suala la uchomaji majengo ya shule linakomeshwa na hata wakibainika sheria ichukue mkondo wake na hatua kali zichukuliwe dhidi yao," alisema.

Zacharia Mushi, alisema uharibifu wa miundombinu unaofanyika kwenye majengo ya shule unarudisha nyuma maendeleo yao ya elimu, kwa kuwa wanafunzi wengi muda wote wanakuwa kwenye wasiwasi wa kutokea majanga.

Mkurugenzi wa Idara ya Watoto Jimbo la Dodoma Kati, Kanisa la Tanzania Assemblies of God, Mchungaji Marcel Mushi, aliwataka wanafunzi kuendelea kuiomba serikali kujenga shule na mabweni yanayohujumiwa kwa wakati.

Aidha, aliwaomba wanafunzi hao kutokatishwa tamaa kutokana na hujuma hizo zinazofanywa, bali kinachotakiwa ni wao kuhakikisha wanatoa ushirikiano kwa serikali ili kuwabaini na kuwachukulia hatua wahalifu.

"Mnachotakiwa kufanya ni kuendelea kusoma kwa bidii na kuipa ushirikiano serikali kwa kutoa taarifa za watu hawa, ambao wanajihusisha na uchomaji wa mabweni na madarasa katika shule zetu," alisema.



Mafundi katika ofisi za Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Dodoma wakijadili na kutengeneza moja ya mitambo aina ya Caterpillar D40 inayotumika katika shughuli za ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walia kisa wageni kufanya biashara za Wamachinga

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

JUMUIYA ya Wafanyabiashara Tanzania imeiomba serikali kuwasaidia wafanyabiashara wadogo ambao hivi sasa shughuli zao zimechukuliwa na raia wa kigeni hasa maeneo ya Kariakoo, jijini Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Siliva Kyando, alitoa ombi hilo kwenye mkutano mkuu wa wenyeviti na makatibu wa jumuiya kutoa mikoa yote uliofanyika juzi jijini hapa.

Kyando, aliiomba serikali kuwazuia wafanyabiashara wa Kichini kuingilia biashara ya wamachinga kwa sababu kufanya hivyo inawaondolea ajira kundi hilo.

"Hatuwazuii Wachina kufanyabiashara nchini, tunachopinga ni kuendelea kuingilia biashara ya wamachinga baadala ya kuwazuia wachuuzi hao ili wapate ajira," alisema.

Alibainisha kuwa Wachina hao wanafanya mazingira ya biashara kwa wamachinga hususani wa Kariakoo kuwa magumu kutokana na kuingia kuuza mitaani.

Kyando alisema wafanyabiashara wa Kichina wanaagiza mzigo kutoka kwao na wengine wanapata mikopo yenye riba nafuu huko kwao, hivyo wakileta biashara nchini wanao uwezo wa kuuza bei ya chini kuliko mfanyabiashara mzawa.

Aidha, jumuiya hiyo ilisema Wachina wanafanya biashara za kichuuzi ambazo zinafanywa na wafanyabiashara ndogo, hivyo kufanya mazingira kuwa magumu kwa wazawa.

"Tunawapenda Wachina ni marafiki zetu wa muda mrefu, lakini hatutaki kuingiliwa soko letu, wao ni wawekezaji siyo kuja kufanya biashara ambazo wamachinga wanazifanya," alisema Kyando.

Hata hivyo, mwenyekiti huyo alisema wanaamini serikali ya awamu ya tano ni sikivu, itashughulikia tatizo hilo kwa wafanyabiashara.

Kadhalika, Kyando aliiomba serikali kuwatafutia maeneo maalum wamachinga wazawa ili kuondoa migongano na wenye maduka makubwa kutokana na kupanga bidhaa zao mbele yao.

"Unakuta Mmachinga kapanga bidhaa zake mbele ya duka ambalo na lenyewe lina uza bidhaa kama hizo, hivyo hali hiyo imekuwa ikileta mtafaruku kati ya wenye milango ya maduka na kundi hilo," alisema.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Biashara la Taifa, Dk. Godwin Wanga, alisema serikali ipo pamoja na wafanyabiashara wazawa na matatizo hayo yatashughulikiwa.

Alisema serikali inatoa vibali kwa wafanyabiashara wote, lakini wageni wanatakiwa kuendesha biashara kubwa na ndogo zinatakiwa kufanywa na wazawa.

Aliitaka jumuiya hiyo kuisaidia serikali kutoa elimu kwa wenzao kulipa kodi ili kuongeza mapato.

HABARI MBEYA

# Wenyeviti walalamikia hospitali Mbarali tozo kwa kinamama

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

WENYEVITI wa vitongoji katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wamelalamikia watumishi wa hospitali ya wilaya hiyo kuwatoza Sh. 50,000 kinamama wanaokwenda kuwapima watoto kliniki.

Kutokana na hali hiyo, wenyeviti hao waliwaomba viongozi wa mamlaka na halmashauri kulifuatilia kwa karibu suala hilo, ili kuchukua hatua kwa wahusika na kukomesha tabia hiyo.

Wakizungumza juzi kwenye kikao cha Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa, wenyeviti hao walisema suala hilo ni kinyume cha taratibu za maadili ya kazi na kama ni njia ya kutaka kukomesha tabia ya kinamama kuacha kujifungulia nyumbani, watafute njia nyingine, lakini sio kuwatoza kiasi hicho kikubwa cha fedha.

Hawa Msigwa wa Kitongoji cha Muungano, alisema alipokea malalamiko kutoka kwa kinamama wa eneo lake kwamba wanapofika hospitali ya wilaya wanaambiwa walipe kiasi cha fedha Sh. 50,000 ndipo wapewe huduma za kupima watoto.

Msigwa alisema kiasi hicho cha fedha wanachotozwa kinadaiwa ni faini kwa kinamama ambao walizalia nyumbani, jambo ambalo alidai ni kinyume cha maadili ya kazi.

"Kuna tabia ya wahudumu wa hospitali ya wilaya kuwatoza kinamama waliozalia nyumbani kiasi cha shilingi 50,000 kama faini, na kama mtu hana hapewi huduma, tunaomba viongozi ufumbuzi wa hili maana kama wanatoa, je, imepishwa na nani?" Alihoji Msigwa.

Goden Mgombavanu wa Nyaruhanga 'B', alisema suala la kinamama kutozwa faini lipo na linalalamikiwa, hivyo ili kukomesha tabia hiyo waitwe wataalamu wote wa afya katika hospitali hiyo wapewe adhabu au karipio.

Kaimu Ofisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo Rujewa, Tuntufye Chamba, aliwaomba wenyeviti hao kuwa tayari kutoa ushahidi utakapohitajika watakapowaita watumishi wa hospitali hiyo kuhojiwa.

Chamba alisema endapo suala hilo linafanywa na watumishi wa afya sio la maadili, hivyo atakayebainika anapaswa kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

Mwenyekiti wa Mamlaka hiyo, Chameta Godigodi, aliwaomba wenyeviti hao kutosubiri vikao ndipo wawasilishe malalamiko hayo ambayo yanagusa moja kwa moja maisha ya watu, badala yake wafikishe kwenye mamlaka husika ili hatua zichukuliwe mapema.

Alisema kutokana na watumishi kulalamikiwa kuwatoza kinamama fedha ndipo wapate huduma halikubaliki, na kwamba uongozi wa Wilaya pamoja na mganga mkuu wa wilaya hiyo watafikishiwa malalamiko hayo.

Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya hiyo, Oliver Sulle, aliwashukuru wenyeviti kwa kuliwasilisha suala hilo kwenye vikao na kuwahakikishia kuwa wilaya itakwenda kufanya vikao vyake pamoja na uchuguzi ili kukomesha tabia hiyo.

Alisema halmashauri haina taarifa yoyote na wala haijabariki wataalamu wa afya kuwatoza kinamama fedha kwa ajili ya kliniki ya watoto, bali wanafanya kwa matakwa yao ambayo ni kunyume na sheri za utumishi wa umma.



Ofisa Ufuatiliaji wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Moris Momba, akitoa maelekezo kwa wawezeshaji wa mfuko huo, wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, kwa ajili ya kwenda kufuatilia taarifa za wanufaika. **PICHA GRACE MWAKALINGA**.

# TMDA yawahakikishia usalama jamii

**Na Grace Mwakalinga,**

**MBEYA**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imewahakikishia wananchi kuwa itaendelea kulinda afya ya jamii dhidi ya watu wanaokiuka sheria na kuhatarisha maisha.

Imesema itatekeleza hilo kwa kudhibiti ubora na usalama wa dawa na vitendanishi katika maeneo ya mipakani.

Mratibu wa Ofisi za Kanda za TMDA, Dk. Henry Irunde, aliyasema hayo juzi wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya wakaguzi wa dawa ngazi ya halmashauri ambayo yaliwahusisha waganga wakuu, wafamasia na madaktari wa binadamu na mifugo kutoka halmashauri na wilaya zote za Mkoa wa Mbeya.

Irunde alisema moja ya majukumu waliyonayo sasa ni kuhakikisha wanalinda afya za wananchi kwa kudhibiti uingizwaji wa dawa au vifaa tiba vyenye athari kiafya pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kutambua bidhaa feki na zilizokwisha muda wa matumizi.

Alisema hadi sasa asilimia 80 ya dawa na vifaa tiba vinavyotumika vinaagizwa nje, hivyo jukumu lao ni kuhakiki ubora kabla ya wananchi kuanza kutumia.

Aliwaomba wakaguzi 57 ambao walijengewa uwezo wa namna ya kufanya ukaguzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, kuzingatia maadili ya kazi katika kukabiliana na vifaa tiba bandia na utoaji wa taarifa kuhusiana na bidhaa hizo.

Kaimu Meneja wa TMDA, Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Anitha Mshighati, alisema moja ya mikakati waliyoiweka ni kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika mipaka ya Tunduma na Kasumulu ili kudhibiti uingizwaji wa dawa bandia.

Alisema kwa kuwa wakaguzi hao ni watendaji wa halmashauri, anaamini baada ya mafunzo hao watakwenda kukabiliana na kudhibiti mianya yote ilikuwa inatumika kuingiza bidhaa zilizopigwa marufuku.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Agness Buchwa, alisema uwekezaji wa viwanda vya vifaa tiba utasaidia kupunguza tatizo la dawa na vitendanishi bandia nchini.

Alisema hadi sasa Mkoa wa Mbeya una jumla ya viwanda vitatu vya kutengeneza vitakasa mikono ambavyo kimsingi havikidhi mahitaji na kwamba hitaji ni ujenzi wa viwanda vya kutengeneza dawa.

Aliwaomba wawekezaji kuchangamkia fursa ya uwekezaji katika dawa ili kukabiliana na tatizo ya bidhaa zilizopigwa marufuku ili kuokoa maisha ya wananchi.

Mmoja wa wakaguzi waliopata mafunzo hayo, Mganga Mkuu Hospitali ya Wilaya ya Chunya, Dk. Felister Kisandu, alisema ameongeza maarifa ya kubaini upungufu uliyokuwa kwenye dawa, hivyo atakwenda kutoa elimu kwa wananchi kuacha matumizi ya dawa ambazo zilipigwa marufuku au kumaliza muda wake.

James Mwangolombe, mfamasia wilayani Kyela, alisema moja ya matatizo yanayokwamisha utendaji kazi wilayani humo ni uingizwaji bidhaa kwa njia za panya.

# Wakulima kupatiwa teknolojia kubadili mabadiliko tabianchi

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

KUTOKANA na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira, watafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kituo cha Uyole, wameamua kusambaza kwa wakulima teknolojia ya kilimo hifadhi.

Lengo la hatua hiyo ni kuwasaidia walioathiriwa na kuongeza uzalishaji wa chakula.

Hatua hiyo ilitangazwa na Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, wakati akizungumza na Nipashe juu ya mipango waliyoiweka katika kuwasaidia wakulima kukabiliana na mabididiliko ya tabianchi msimu huu wa kilimo ambao umeanza.

Alisema wakulima wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ya Rukwa, Iringa, Mbeya na Katavi wameshaanza kuona mafanikio kwani wameanza kutumia uhifadhi wa rasilimali udongo na mazingira katika maeneo yao.

Aliongeza kuwa kilimo hicho kinafuata kanuni kwa kulima kilimo cha mzunguko cha mazao ya nafaka na mikunde ambayo yamekuwa yakiongeza mbolea na uhifadhi wa udongo katika shamba.

"TARI Uyole imeamua kuhimiza kilimo hifadhi kwa sababu kinaongeza uzalishaji kwenye maeneo yenye ukame. Pia kina wahakikishia wakulima usalama wa chakula pamoja na kupunguza gharama za uzalishaji, hivyo kuongeza kipato kwa mkulima," alisema Dk. Bucheyeki.

Aliongeza kilimo hifadhi pia kinasaidia kupunguza muda wa kufanya kazi shambani, hivyo mkulima anapata muda wa kufanya shughuli zingine za maendeleo pamoja na kudhibiti mmomonyoko wa udongo na kumudu mabadiliko ya tabianchi.

Pia alisema kilimo hifadhi kinakabiliwa na vikwazo mbalimbali ukiwamo uhaba wa wataalamu wa kilimo wenye elimu ya kilimo hifadhi, huku akieleza bado eneo linalolimwa kwa kilimo hicho ni dogo ambapo mpaka mwaka 2012 ni ekari 62,500 tuu ndizo zilitumia teknolojia hiyo.

Alisema TARI imejipanga kuhakikisha teknolojia zinazozalishwa zinasambazwa na kuwafikia wakulima na wadau wengine wa kilimo ili kuongeza uzalishaji wa malighafi za zinazotokana na kilimo zinazohitajika katika uchumi wa viwanda.





# Wakulima wa nyanya walia kukosa soko

**Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKULIMA wa nyanya Zanzibar walalamikia kushuka kwa bei ya soko la zao hilo.

Hali hiyo imesababishwa na hoteli nyingi za kitalii kufungwa kutokana na janga la ugonjwa wa corona duniani.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakulima hao walisema nyanya hazina soko, hali ambayo imepelekea kuuza kwa bei ndogo kutokana na wingi wa nyanya uliopo.

Alisema tenga moja la nyanya lililokuwa likiuzwa Sh. 45,000 hivi sasa wanalazimika kuuza kwa Sh. 25,000 ili zisije kuwaozea mashambani.

Ali Khamis ni mkazi wa Shakani, alisema kuwa wananchi wa Zanzibar walihamasika kulima kilimo hicho baada ya kuwa na bei nzuri hasa katika hoteli za kitalii.

Alisema hivi sasa nyanya zinalimwa kwa wingi Zanzibar na imeacha kutegemea soko la nyanya kutoka Tanzania Bara.

Alisema kwa sasa soko hilo limeshuka na kupelekea kupata hasara, ambapo ametumia gharama kubwa katika kilimo hicho.

"Bado soko la nyanya halijawa zuri tokea kuibuka kwa maradhi ya corona kwa sababu bado hoteli nyingi za kitaili hazijafunguliwa licha ya kwamba baadhi tu ya hoteli ndizo zilizofunguliwa, baada ya kupata wageni," alisema.

Alieleza kuwa soko la nyanya kwa sasa ni kwa ajili ya mahitaji ya kawaida ya wananchi, lakini kungekuwa na kiwanda cha kuchakata nyanya soko la zao lisingeshuka.

Asha Bakari, mkaazi wa Kombeni, alisema kukosekana kwa ushirika au jumuiya ya wakulima wa nyanya na mboga kunaathiri sana mfumo wa bei wa mazao hayo.

Alisema kama kungekuwa na umoja au ushirika wa wakulima wa nyanya, wangeweza kudhibiti soko la bei la zao hilo.

Alizitaka taasisi za kibenki ziangalie masharti ya mikopo kwa wakulima na masharti waliyoweka yamepelekea wakulima hasa wa nyanya kutokopesheka.

"Tunaziomba taasisi za kibenki zipunguze masharti ya mikopo, ili na sisi tupate kukopa fedha kwa ajili ya kuendeleza kilimo chetu," alisema.

Ofisa uwezeshaji kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) ofisi za Zanzibar, Nairat Abdallah, alisema wakulima wa mboga wanahitaji kupata mikopo kuendeleza kilimo, lakini wanashindwa kutokana na masharti makubwa ya vitu vya thamani.

"Ni kweli ukitaka kukopa benki moja ya masharti uwe na vitu vya thamani (dhamana), aidha nyumba au gari, jambo ambalo ni gumu kwa wajasiriamali wetu hasa wakulima," alisema.

Aliwataka wakulima hao licha ya changamoto zinazowakabili, wasivunjike moyo na waendelee na harakati zao za kilimo kwa sababu kilimo ni uti wa mgongo.

Alieleza kuwa TAMWA kwa kushirikiana na wadau wengine wanatarajia kulifufua soko la wazi la wajasiriamali ambalo lilikuwa likifanyika kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi, lakini lilisitishwa kutokana na corona.



Baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wakimsikiliza Spika wa Baraza hilo, Zuberi Ali Maulid (hayupo pichani), katika semina maalum kuhusu uundwaji wa kamati za baraza. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wazalishaji mwani waomba bei nzuri

**Na Mwandishi Wetu,** Pemba

WAKULIMA wa mwani Mkoa wa Kaskazini Pemba wameliomba shirika la ununuzi wa mwani kuongeza bei ya zao hilo, ambayo itaendana na hali halisi ya maisha.

Walisema kuwa ni vyema shirika kuwaongezea bei wakulima wa zao hilo kutoka Sh. 600 kwa kilo moja hadi angalau Sh. 1,500, ili kuwasaidia katika kutatua shida zao zinazowakabili.

Hayo yalielezwa na baadhi ya wananchi wa maneo tofauti wa mkoa huo, walipokuwa wakizungumza na waandishi wa habari.

Rahma Salim Abdalla, mkaazi wa Tumbei, alisema lengo la kuomba kuongezewa bei ya mwani, ni kutokana na kazi kubwa wanayoipata kwenye kilimo hicho.

"Kilimo cha mwani ni kama kilivyo kilimo kingine, isipokuwa tu mwani unakuwa na majukumu makubwa zaidi toka kupandwa hadi kufikia kuvunwa," alisema mkulima huyo.

Alisema kilimo cha mwani kimekuwa na tija na faida kwa wananchi wa Zanzibar na kimekuwa kikiwasaidia kujipatia fedha ambazo zimekuwa zikiwasaidia katika kutatua shida zao.

Asha Asaa Sheha, mkulima wa mwani, mkaazi wa Tumbe Magharibi, alisema kilimo cha mwani ni chenye tija, lakini kina kazi kubwa toka kuanza hadi kufikia kuvuna.

"Kilimo cha mwani kimekuwa na faida kubwa kwa jamii, lakini hususani kwa sisi kinamama na vijana... tumeweza kujikomboa kiuchumi na kuondokana na umaskini kutokana na juhudi zetu kwenye kilimo cha mwani," alisema.

Ramla Amour Abdalla, mkaazi wa shehia ya Tumbe Mashariki, alieleza kuwa kilimo hicho kinachangamoto kubwa ya kipekee kuliko hata kilimo kingine.

# Spika sasa awapa 'meno' Wawakilishi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid, aliwataka wajumbe wa baraza hilo kuchangia mambo mbalimbali katika baraza hilo kwa uwazi bila hofu.

Alisema katika baraza lililopita baadhi ya wajumbe walikuwa waathirika kwa sababu ya kuzungumzia madudu yaliyomo ndani ya serikali na baadhi yao waliitwa mpaka katika tume ya maadili ya chama kwa kuonekana kuwa wameikosoa serikali wakati wajumbe wapo sahihi.

"Niwaambieni kuwa msiwe na hofu ya kuchangia, kuweni wawazi na msiwe na wasiwasi kwa sababu Rais wetu anapenda kuibuliwe changamoto zilizopo ili zifanyiwe kazi, "alisema Spika Zuberi.

Alibainisha hayo jana wakati wakichangia katika semina kuhusu uundaji wa kamati za baraza hilo.

Miongoni mwa mapendekezo yao ni kutaka kuchunguzwa majengo ya miradi ya maendeleo kwa sababu baadhi ya majengo hayo ya serikali yanayojengwa hayana kiwango bora. Hamza Hassan Juma wa Jimbo la Shaurimoyo, alisema uendeshaji wa meli ya abiria ya Mapinduzi ni hasara kwa sababu meli hiyo imeletwa ikiwa na mashine mbovu. Alisema matatizo ya meli ya M.V Mapinduzi namba mbili yalifahamika mapema na kamati ya Baraza la Wawakilishi kuiwasilisha serikalini, lakini hakuna hatua zozote zilizochukuliwa na matokeo yake yamebainika hivi karibuni.

Alisema hata mradi wa kutotoa vifaranga vya samaki uliopo Beit-el-Ras, kamati iligundua udhaifu wake na kutoa taarifa yake serikalini, lakini hata hivyo hakuna hatua zaidi zilizochukuliwa za ufuatiliaji.

Alisema hayo yote yamejitokeza kutokana na serikali kushindwa kuzifanyia kazi taarifa za kamati za Baraza la Wawakilishi ambazo miongoni mwa majukumu yake ni kuibua miradi yenye kasoro na serikali kazi yake kuzifanyia kazi.

Alisema madudu yanayoibuliwa hivi sasa na mawaziri wapya kuhusiana na miradi mbalimbali ya maendeleo, inaonekana kama wajumbe wa Baraza la Wawakilishi lililopita kuwa halikufanya kazi.

Akiwasilisha mada kuhusu ushirikishwaji wa wananchi na wadau katika kamati za Baraza la Wawakilishi, Mshauri wa Sheria wa Baraza hilo, Mussa Kombo Bakari, alisema kuna changamoto katika kuwashirikisha wananchi, asasi za kiraia katika kamati ni kukosa umakini miongoni mwa jumuiya za kiraia na kushindwa kutumia fursa ya kushirikiana na kamati za baraza.

Alisema baadhi ya kamati hukosa umakini na kushindwa kutumia vizuri maoni ya wananchi na jumuiya za kiraia. "Ufinyu wa bajeti unaozifanya kamati kushindwa kuwafikia wananchi wengi zaidi Unguja na Pemba na kukosekana kwa utaalamu kwa baadhi ya fani miongoni mwa wananchi," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam - 0768 928 516.**
**Arusha - 0677 226 960.**

## NAFASI ZA MASOMO

**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** ILIYOPO SALASALA RTD INATANGAZA NAFASI ZA AWALI NA MSINGI. KWA MAWASILIANO **PIGA SIMU: 0713 327613.**

*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUFUNGWA KWA KAMAPUNI 131428

**AABHA INTERNATIONAL LIMITED**
**P O BOX 642 MWANZA**
**MOBILE 0787810101**

**BOARD RESOLUTION**
**SHAEHOLDERS' RESOLUTION APPROVING DISSOLUTION OF THE COMPANY**
Name of the company : **AABHA INTERNATIONAL LIMITED**
Registered address: **P O BOX 641 MWANZA**

At a meeting of the Directors held at 08:00 am. 10:00 am on 25/12/2017 The following resolution was passed.

The shareholders of the company hereby dissolve the company with effect from 30/12/2017

**NOW THEREFORE BE IT RESOLVED** that the company shall wind up its affairs,and the company shall be dissolved.

AABHA INTERNATIONAL LIMITED
P.O. Box 642
MWANZA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi No;347/2020 Ombi la **ADAM PETER LIUNJI**,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **PETER STEVEN LIUNJI.** Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **16/12/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **16/11/2020.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**BEATRICE ELIOTH MAHALI** anatangaza kupotelewa na vyeti. Cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0500-0016** kilichotolewa na **WANIKE SEKONDARI** mwaka 2010. Certificate in Records Management chenye namba **DRM. 01/14/T.35** kilichotolewa na Chuo cha Utumishi wa Umma **(TABORA)** mwaka **2014.** Diploma in Records Management chenye namba **DRM.01/14/T.35** kilichotolewa na Chuo cha Utumishi wa Umma **(TABORA)** mwaka 2015.

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha Polisi.**
**Control No. 9910819688147.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**EFFCO SOLUTIONS (T) LTD** inatangaza kupotelewa na kadi za magari.
Kadi ya Gari namba **T 238 BMM CATERPILLAR,** Kadi ya Gari namba **T 114 DCG MERCEDEZ BENZ,** Kadi ya Gari namba **T 156 CAG CATERPILLAR,** Kadi ya Gari namba T 245 BMM CATERPILLAR, Kadi ya Gari namba T 352 DCF CATERPILLAR.

**Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.**
**Control No: 9910819761744.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGRO**
**MAOMBI NA.297 YA MWAKA 2020.**

**HALID ATHUMANI MAGANGA...............**
**MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**SAID NASSORO**
**EFRAIM S. WAPALILA**
**ALMAS CHARLES MVUNGI............MJIBU MAOMBI**
**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**SAID NASSORO**

Popote Ulipo Unaarifiwa Ufike ktk baraza la Ardhi na Nyumba la wilaya ya Morogoro tarehe 08/12/2020 mwenyewe binafsi au mtume mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautaudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa mkono wangu leo tarehe 9 Mwezi November,2020.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

***JAMAL SWALEH RASHID*** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HARRIER** chasis namba **ACU3000059255**,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Polisi taarifa**
**DOD/DOD**
**RB/824993/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

LEOPODI PATRICK KIMARO anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya STAR yenye namba za usajili MC449AYU. Chassis namba LTZPCK-LN5D6101917 na Engine namba 162FMJD0003042. Yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Taarifa ya polisi:
**MAN/BAB/R-B/805159/2020.**

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**
**SHAURI NO.130/2020**
**MAHONA LATU MBUSA........................MDAI**
**Versus**
**GUNGWA MAHEGA....................................MDAIWA**
**TENGE GUNGWA MAHEGA........................MDAIWA**
**SHINGE TENGE GUNGWA.........................MDAIWA**
**YAH:KUITWA SHAURINI**

**KWA:**
**SHINGE TENGE GUNGWA,**
Fahamu kwamba **MAHOMA MBUSA** amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe **14/12/2020** saa **3:00** asubuhi mbele ya Mh.A.Mapunda Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleya utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka: Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/ Muhuri wa baraza hili leo tarehe **16/11/2020.**

**A.Mapunda**
**MWENYEKITI**
**16/11/2020**

## KUPOTEA KWA VYETI



**STEWARD CYPRIAN BUCHA** anatangaza kupotelewa kwa vyeti,cha kidato cha nne index namba **S.1571/0079** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **BUSEKO HILL** mwaka **2017,** result slip ya kidato cha sita na leaving certificate index namba **S.2211/0532** shule ya **MWILAMVYA** mwaka 2020,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Polisi taarifa**
**DAR/MSI/RB/824900/2020**

## KUFUNGWA KWA KAMAPUNI 69098

**UMEME SOLUTIONS LIMITED**
**P O BOX 541 MWANZA**
**MOBILE 0683230099**

**BOARD RESOLUTION**
**SHAEHOLDERS' RESOLUTION APPROVING DISSOLUTION OF THE COMPANY**
Name of the company : **UMEME SOLUTIONS LIMITED**
Registered address: **P O BOX 541 MWANZA**

At a meeting of the Directors held at 08:00 am. 10:00 am on 15/05/2010 The following resolution was passed.

The shareholders of the company hereby dissolve the company with effect from 30 JUNE 2010

NOW THEREFORE BE IT RESOLVED that the company shall wind up its affairs,and the company shall be dissolved.

UMEME SOLUTIONS LIMITED
P.O. Box 541
MWANZA

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Rais Museveni ashutumu upinzani

**Kampala,** UGANDA

RAIS Yoweri Museveni wa Uganda, ameshutumu waandamanaji na wanasiasa wa upinzani kwa kuwapotosha vijana kujiingiza katika vitendo vya uhalifu.

Museveni (pichani) alisema wazo la kuwa Mheshimiwa Bobi Wine kukamatwa kutakuwa na ghasia, lisirejee tena.

"Hakuna mwanasiasa ambaye ana mamlaka kuliko sheria," Museveni alisema.

Aliongeza kuwa wanasiasa wanalipa magenge ya uhalifu ambao wametangaza baadhi ya sehemu za mji wa Kampala, kwamba hazitawaliki na hata kuvamia maofisa wa polisi wanaoshika doria.

**Wazo la kuwa Mheshimiwa Bobi Wine kukamatwa kutakuwa na ghasia, lisirejee tena.**



Museveni alishutumu watu waliorekodiwa wakivamia maofisa wa usalama na waliokuwa wamevaa mavazi ya rangi ya njano inayoashiria chama tawala.

"Hili, halitawahi kutokea tena, kwa sababu waliotekeleza hayo wameona matokeo ya kucheza na moto," alisema Rais Museveni.

Pia alisema ajenda za wanasiasa wa upinzani kupata uungwaji mkono kutoka nje ya nchi ambao nia yao ni kukosesha uthabiti nchi ya Uganda.

Rais Museveni aliongeza kuwa makosa makubwa ni wagombea urais walikiuka hatua zilizowekwa za kukabiliana na virusi vya corona na kutojali utekelezaji wa sheria.

Alitoa risala zake za rambirambi kwa raia wa Uganda, waliopoteza wapendwa wao wakati wa ghasia hizo na kuongeza kwamba serikali itawalipa fidia.

Bobi Wine anatafuta kumwondoa madarakani Rais Museveni, ambaye ametawala nchi hiyo kwa miaka 34 katika uchaguzi utakaofanyika Januari 2021. **BBC**

## Sitobadilisha msimamo wangu kwa miezi 6-Trump

**Washington,** MAREKANI

RAIS anayemaliza muda wake nchini Marekani, Donald Trump (pichani chini), amesema kamwe hatobadilisha msimamo wake juu ya mashtaka yake bila uthibitisho wa wizi wa kura.

Alisema hayo katika mahojiano yake ya kwanza ya runinga, tangu Joe Biden kutangazwa mshindi wa uchaguzi.

"Hakuna mtu ambaye anaweza kunibadilisha mawazo yangu. Sitobadilisha mawazo yangu kwa kipindi cha miezi sita," Rais Donald Trump amekimbia kituo cha Fox News.

"Uchaguzi huu uligubikwa na wizi wa kura," alisema bila kutoa ushahidi wowote. Tulishinda kwa kiasi kikubwa."

Hayo ni mahojiano yake ya kwanza tangu kufanyika kwa uchaguzi wa urais Novemba 3, mwaka huu.

Licha ya shutuma za mara kwa mara za bilionea huyo wa Marekani, mawakili wake wameendelea kushindwa katika mahakama mbalimbali nchini humo, wakijaribu kuonyesha jinsi uchaguzi huo wa urais ulivyogubikwa na udanganyifu mkubwa.

"Tunajaribu kuonyesha ushahidi, lakini majaji hawaturuhusu," alisema Donald Trump. Tunajaribu. Tuna ushahidi mwingi."

Akipuuzia uhuru wa mahakama, Rais wa Marekani ameilalamikia Wizara ya Sheria na Shirika la ujasusi la Marekani la FBI kutomuunga mkono. **RFI**





Wakazi wa Jiji la Sydney nchini Australia, wakiwa ufukweni mwa bahari kupata ahueni baada ya kiwango cha juu cha joto kufikia nyuzi 40 juzi (Jumapili), siku chache kabla ya kuanza majira ya joto. **PICHA: MTANDAO**

## Sydney yashuhudia kiwango cha juu joto

**Sydney,** AUSTRALIA

JIJI la Sydney nchini Australia, limeshuhudia kiwango cha juu cha joto kilichofikia nyuzi 40, ikiwa ni siku chache kabla ya kuanza majira ya joto.

Aidha, maeneo tofauti yaliyo na msitu yamekuwa yakiwaka moto huko New South Wales, huku utabiri wa hali ya hewa ukionyesha ongezeko la joto, siku ya leo.

Mkuu wa Kituo cha Hali ya Hewa, Andrew Watkins (BOM), alinukuliwa mwishoni mwa wiki akisema:

"Novemba imekuwa si ya kawaida tumeshuhudia mvua chache, isiyo kawaida na itakuwa ni mwezi wa kipekee," alisema Watkins.

Pia majimbo ya Victoria na Australia Kusini pia yaliripoti kuongezeka kwa joto mwishoni mwa wiki.

Kumekuwa na matukio ya picha tofauti ambazo zinaonyesha makundi ya watu wakipumzika kwenye fukwe za bahari.

Idara za afya eneo la New South Wales zimesisitiza kuwepo kwa angalizo la kuepuka msongamano ili kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona.

Naibu Kamishna wa Huduma za Moto Vijijini (RFS), Peter McKechnie, alisema watu wawe na mipango ya kukabiliana na moto.

"Hii ni mara ya kwanza tangu msimu wa mwaka jana kuona hatari kubwa ya moto kuweza kutokea," alisema. **BBC**

## Iran yamzika mwanasayansi nyuklia

**Dubai,** U.A.E

IRAN imefanya mazishi ya mwanasayansi wa nyuklia aliyeuawa mwishoni mwa wiki, Mohsen Fakhrizadeh katika makaburi yaliyopo kaskazini mwa Tehran.

Televisheni ya serikali iliripoti, huku waziri wa ulinzi akiahidi Jamhuri ya Kiislamu italipiza kisasi kwa mauaji hayo. Fakhrizadeh, amekuwa akishukiwa kwa muda mrefu na nchi za Magharibi na Israeli, kwamba anasimamia mpango wa siri wa silaha za nyuklia.

Mwanasayansi huyo alishambuliwa kwa risasi akiwa katika gari lake, Ijumaa kwenye barabara kuu, karibu na Tehran.

Wakuu wa makasisi na viongozi wa kijeshi wa Iran wameilaumu, Israel, kwa mauaji hayo. Iran pia iliwahi kuishutumu Israeli kwa mauaji ya wanasayansi kadhaa wa nyuklia mwaka, 2010.

Televisheni ya Serikali iliyonyesha jeneza la Fakhrizadeh, lililofungwa na bendera ya Iran, katika shughuli za mazishi huku viongozi wakuu wa kijeshi, na familia wakihudhuria. **REUTERS**

# MESSI ATOA USHINDI KWA MARADONA




**BARCELONA,** Hispania

NYOTA wa Barcelona na Argentina, Lionel Messi, alitoa heshima kwa gwiji wa zamani wa timu hizo, Diego Armando Maradona ambaye alifariki dunia mwanzoni mwa juma hili.

Messi mwenye umri wa miaka 33, alitoa heshima hiyo baada ya kufunga goli la mwisho kwenye ushindi wa 4-0 dhidi ya Osasuna uliopigwa dimba la Camp Nou, Jumapili kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Baada ya kufunga bao hilo, Messi alivua jezi akibakia na ile ya ndani ambayo ilikuwa inaonyesha timu ambayo alianzia soka lake, lakini ni miongoni mwa timu bora za muda wote ya Maradona nchini Argentina.

Mabao mengine kwenye mchezo huo yalifungwa na Martin Braithwaite, Antoine Griezmann na Philippe Coutinho kukamilisha ushindi huo mnono.

Maradona, miongoni mwa wachezaji bora duniani alifariki dunia Jumatano iliyopita akiwa na umri wa miaka 60.

# Mourinho akunwa na wachezaji kuchukia sare

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amebainisha wachezaji wa Tottenham Hotspur hawakuwa na furaha baada ya sare ya bila kufungana na Chelsea, kitu ambacho kocha huyo wa Spurs amekitaja kama "kubadilika kwa akili".

Spurs ilirudi kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England – kwa tofauti ya mabao baada ya sare hiyo tasa pale kwenye dimba la Stamford Bridge, Jumapili.

Tottenham, ambao walishinda 2-0 dhidi ya Manchester City katika mchezo uliopita kwenye Ligi Kuu, walipiga mashuti matano tu golini, huku moja likilenga goli, likipigwa na Serge Aurier dakika ya 15.

Chelsea kwa upande mwingine walipiga mashuti 13 golini, huku Hugo Lloris akiokoa hatari tatu, mbili za Mason Mount na moja ya Olivier Giroud.

Na baada ya mchezo huo, Mourinho alisema anajisikia furaha kuona kwamba wachezaji wake wamebadilika kiakili kwa kuonyesha kutopendezwa na matokeo hayo.

"Kitu kimoja nilichokichukua kutoka kwenye mchezo huu ni kwamba, sare kwa kawaida ni matokeo chanya," alisema Mourinho akiiambia Sky Sports.

"Nilichokipenda zaidi ni kwamba, wachezaji walionyesha kutokuwa na furaha kwenye vyumba vya kubadilishia nguo kutokana na sare ile, hicho ndicho kitu bora kwangu nilichokichukua katika mchezo ule."






# *Gattuso: Inter itatwaa ubingwa wa Serie A*

**NAPLES,** Napoli

KOCHA Mkuu wa Napoli, Gennaro Gattuso, anaamini Inter Milan ina nafasi kubwa ya kushinda taji la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, msimu huu, mbele ya vinara wa sasa, AC Milan na bingwa mtetezi, Juventus.

Milan - ambayo haijatwaa ubingwa huo maarufu kama Scudetto tangu msimu wa 2010-11, ipo kileleni mwa msimamo ikiongoza kwa pointi tano kwa mechi tisa baada ya kuifunga Fiorentina 2-0, Jumapili na kubaki kuwa timu ambayo haijapoteza mchezo msimu huu.

Wapinzani wao wa jiji moja, Inter na Sassuolo wamepitwa pointi tano, huku kikosi cha Andrea Pirlo, Juve kipo nafasi ya nne kikipitwa pointi sita pamoja na Napoli iliyo nafasi tano na AS Roma nafasi ya sita.

Gattuso anaona kwamba, kikosi cha Antonio Conte, Inter kina nafasi kubwa ya kutwaa ubingwa huo, baada ya timu yake ya Napoli kuifumua Roma mabao 4-0 Jumapili, ameiambia Sky Sport Italia: "Kwa mtazamo wangu, Inter ndio wenye nafasi.

"Ukijumlisha ubora na uimara wao dimbani, wana nafasi kubwa mno na kwangu mimi nawapa nafasi ya kulibeba taji hilo.

"Halafu kuna Juventus, ambao ni kawaida yao kuwa pale, hivyo mbio za ubingwa wa msimu huu zitakuwa za nguvu kwelikweli."

Napoli imecheza mchezo wake wa kwanza kwenye Serie A tangu kifo cha gwiji wa klabu hiyo, Diego Maradona Jumatano iliyopita, walicheza kwa hisia kubwa pale kwenye uwanja wa San Paolo, ambapo nahodha wake, Lorenzo Insigne alifunga pamoja na Fabian Ruiz, Dries Mertens na Matteo Politano.

# Cavani aing'arisha Man United

**MANCHESTER,** England

EDINSON Cavani alitokea benchi kuiokoa Manchester United na kipigo wakati mabao yake mawili yalipowawezesha kuibuka na ushindi wa 3-2 dhidi ya Southampton kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Jumapili.

Katika mchezo huo uliopigwa dimba la St Mary's, Southampton walitangulia kujipatia mabao 2-0 hadi mapumziko, lakini usajili mpya, Cavani aliwafanya mashabiki kufurahia baada ya kufunga mabao mawili.

Strika huyo mwenye umri wa miaka 33 raia wa Uruguay, alitumia vema uzoefu wake katika kujipatia mabao yote mawili, yote alikwamisha kwa kichwa akimalizia pasi za Bruno Fernandes na Marcus Rashford.

James Ward-Prowse alianza kuwafunga Man United kabla ya kutengeneza lingine la Jan Bednarek dakika ya 23.

Bao la kwanza la Man United lilifungwa na Fernandes, hata hivyo Kocha Ole Gunnar Solskjaer, alilazimika kufanya mabadiliko kwenye eneo la golikipa baada ya David de Gea kuumia.





# HASSELBAINK AMPA NENO ABRAHAM

**LONDON,** England

STRAIKA wa zamani wa Chelsea, Jimmy Floyd Hasselbaink, amemtaka Tammy Abraham kujiimarisha zaidi ili aweze kupata nafasi ya kucheza zaidi kwenye kikosi hicho.

Abraham alianza wakati Chelsea ikicheza dhidi ya Tottehma Hotspur kwenye mchezo wa Ligi Kuu England katika dimba la Stamford Bridge ambao ulimaliza kwa sare ya bila kufungana, Jumapili.

Latika mchezo huo licha ya Abraham kupata nafasi nyingi za kufunga, lakini hakuweza kufanya hivyo na kujikuta akitolewa nje dakika ya 79.

Nyota huyo wa kimataifa wa England alikuwa nguzo kubwa ya Chelsea wakati wa msimu wa kwanza wa Kocha Frank Lampard, akifunga mabao 15 ya ligi na alitarajiwa kuwa na mafanikio zaidi msimu huu.

Lakini mambo yamekwenda tofauti msimu huu na Hasselbaink sasa anaona ni wakati mzuri kwa straika huyo kujiimarisha ili kuendelea kuwa na namba katika kikosi cha kwanza.

"Anatakiwa kujiimarisha katika nyakati zote. Alifanya vizuri sana msimu uliopita, kwa nusu ya msimu alikuwa kwenye kiwango cha kuvutia, huku akifunga mabao mazuri," alisema Hasselbaink akimzungumzia Abraham na kunukuliwa na Sky Sports.

Hadi sasa msimu huu Abraham ameanza katika mechi nne mfululio za Ligi Kuu na hivyo anaamini anaweza kuendeleza kiwango chake.

"Kipindi cha pili cha msimu uliopita kilikuwa kigumu kwake, lakini ni jambo la kawaida kwa sababu yeye ni kijana, ila msimu huu lazima aimarishe kiwango.

# Tangulia kwa amani Papa Diop, umeacha alama

**LENS,** Ufaransa

NYOTA wa Senegal kwenye Kombe la Dunia mwaka 2002, Papa Bouba Diop, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 42.

Kwa mujibu wa BBC Sport, Diop amefariki dunia baada ya kuugua kwa muda mrefu.

Kiungo huyo wa zamani alicheza katika klabu nne tofauti nchini England, akifurahia wakati wake pale Fulham, Portsmouth, West Ham na Birmingham City baada ya kutamba Lens ya Ufaransa.

Taarifa iliyotolewa kupitia ukurasa wa Twitter wa Lens ilisomeka: "Ni huzuni kubwa kwamba klabu ya Racing Club de Lens imepokea taarifa ya kifo cha mchezaji wake wa zamani, Papa Bouba Diop, akiwa na umri wa miaka 42.

"Tunatoa salamu za pole kwa ndugu na marafiki wake wote kwa kifo hiki."

Diop atakumbukwa zaidi kwa kuisaidia Senegal kutinga robo fainali ya Kombe la Dunia miaka 18 iliyopita.

Alifunga bao pekee wakati walipowafunga bao 1-0 waliokuwa mabingwa watetezi wa Kombe la Dunia, Ufaransa kwenye mchezo wao wa ufunguzi mjini Seoul nchini Korea Kusini.

Alifunga mara mbili wakati wakitoka sare ya 3-3 na Uruguay na Senegal ikafuzu hatua ya mtoano kutoka kwenye makundi kabla ya kuifunga Sweden katika hatua ya 16-bora.

Lakini wakafungwa na Uturuki 1-0 ambao walifuzu hatua ya nusu fainali na Senegal kurudi nyumbani.

Diop alianza kucheza soka nchini Senegal katika klabu ya ASC Diaraf kabla ya kucheza soka la kulipwa nchini Uswisi katika klabu za Vevey, Neuchatel Xamax na Grasshoppers, akishinda taji la Ligi Kuu ya nchi hiyo, Super League mwaka 2001.

Pia alicheza nchini Ugiriki katika Klabu ya AEK Athens, ambapo alishinda kombe la nchini hiyo msimu wa 2010-11, miaka mitatu baada ya kubeba taji la FA akiwa na Portsmouth.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AUBAMEYANG SASA AMPA HOFU ARTETA

## Wote tuna hofu kwa sababu mfungaji mkuu wa mabao wa klabu hafungi wakati huu...

**LONDON,** England

MIKEL Arteta ameonyesha hofu ya kiwango cha Pierre-Emerick Aubameyang baada ya nahodha huyo kuendelea kushindwa kufunga wakati Arsenal ikichezea kichapo kwenye Ligi Kuu England kutoka kwa Wolves.

**Kocha huyo Mkuu wa Arsenal, Arteta amesema kiwango cha Aubameyang ni "hofu kubwa ", akielezea namna gani mabao ya mchezaji huyo wa Kimataifa wa Gabon yalivyo na umuhimu kwa 'Washikabunduki' hao waliopoteza 2-1 nyumbani kwa Wolves, Jumapili.**

Aubameyang alipiga mashuti matano na aligusa mpira mara tisa eneo la penalti kwenye mchezo huo dhidi ya Wolves, lakini shuti moja tu ndio lililolenga goli.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, hajafunga bao la wazi kwenye Ligi Kuu tangu Arsenal ilipoanza msimu huu kwa ushindi rahisi kwa kuwafunga Fulham 3-0 pale kwenye dimba la Craven Cottage, Septemba.

Penalti ya Aubameyang iliwawezesha Arsenal kupata ushindi dhidi ya Manchester United mwanzoni mwa Novemba, lakini mategemeo ya mabao kutoka kwa nyota huyo wa zamani wa Borussia Dortmund yanaonekana kufifia msimu huu.

Alipoulizwa kama anahofia hilo, Arteta alisema: "Nafikiri wote tuna hofu kwa sababu mfungaji mkuu wa mabao kwenye klabu hafungi kwa wakati huu, hivyo jukumu langu kubwa kwa sasa ni namna gani ya kumsaidia yeye afunge mabao kwa sababu tunahitaji mabao yake.

"Namna gani umuhimu wa Auba umekuwapo kwenye klabu hii kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita, yanatuonyesha namna gani mabao yake yalivyo muhimu kwa timu.

"Anahitaji kufunga mabao kama tunataka kupata mafanikio."

Aubameyang alifunga mabao 22 kwa Arsenal kati ya 73 msimu wa 2018-19 wakati walipomaliza nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

Arteta angependa kupata mabao kutoka maeneo yote ya uwanja, lakini ukweli ni kwamba, wanategemea zaidi kiwango bora cha Aubameyang kufunga mabao ili kuweza kuinyanyua timu.

Arsenal ipo nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 13 baada ya mechi 10, ikiwa imepoteza mechi tatu nyumbani mfululizo kwenye mashindano hayo, na wamepitwa pointi nane na vinara Tottenham ambao ni wapinzani wao kutoka London Kaskazini.

## ZISIKUPITE

### KHEDIRA AITAKA EPL

KIUNGO wa Ujerumani, Sami Khedira mwenye umri wa miaka 33, amesema kuhamia Ligi Kuu England linaweza kuwa chaguo lake wakati mkataba wake na Juventus utakapomalizika kipindi cha majira ya joto kijacho. Ameongeza anawasiliana mara kwa mara na kocha wa Everton, Carlo Ancelotti na wa Tottenham, Jose Mourinho. ***(ZDF, via Mail)***

### ANOGEWA AC MILAN

MKATABA wa sasa wa golikipa wa AC Milan, Gianluigi Donnarumma unamalizika mwaka 2021, lakini mchezaji huyo wa kimataif wa Italia mwenye umri wa miaka 21, amesema wakala wake atazungumza na klabu na anataka kubaki na timu hiyo kwa "muda mrefu ". ***(Football Italia)***

### HAINA OFA KWA SCHUURS

LIVERPOOL imekuwa ikihusishwa na mlinzi wa Ajax, Perr Schuurs mwenye umri wa miaka 21, lakini 'Wekundu' hao hawajatoa ofa yoyote kwa raia huyo wa Uholanzi. ***(Voetbal Primeur)***

### MCCARTHY AWANIWA CELTIC

CELTIC inawania kumsajili kiungo wa Crystal Palace na Jamhuri ya Ireland, James McCarthy, lakini Aston Villa na Burnley pia zinawania kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30. ***(Teamtalk)***

### SOLSKJAER HATAKI KUTABIRI

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema hawezi "kutabiri nani ataingia na nani atatoka" wakati wa usajili wa dirisha dogo la Januari. ***(Evening Standard)***

### NYOTA WAPAMBANA BARCA

KIUNGO wa Hispania, Riqui Puig mwenye umri wa miaka 21, na Carles Alena, 22, wanapigania majaliwa yao pale Barcelona pamoja na straika wa Denmark, Martin Braithwaite, 29, na mlinzi wa kushoto wa Hispania, Junior Firpo mwenye miaka 24. ***(Marca)***

### THAUVIN AMTAJA MALDINI

WINGA wa Ufaransa, Florian Thauvin amesema "aliondolewa" na Mkuurugenzi wa Ufundi wa AC Milan, Paolo Maldini, akikubali miamba hao wa Serie A walikuwa wakiwania kumsajili. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, mkataba wake pale Marseille unamalizika kipindi cha majira ya joto 2021. ***(Football Italia)***

### SAVIC AWANIWA JUVENTUS

KLABU ya Juventus inaweza kumwania mlinzi wa kati wa Atletico Madrid na Montenegro, Stefan Savic mwenye umri wa miaka 29, ili kuimarisha safu yao ya ulinzi. ***(Calciomercato)***

### CARLOS NUSURU ATUE CHELSEA

MLINZI wa zamani wa kushoto wa Brazil, Roberto Carlos, amesema dili la yeye kuhamia Chelsea "lilikubaliwa" mwaka 2007, lakini liligonga mwamba "dakika za mwisho". ***(Goal)***

HABARI MICHEZO

## Polisi TZ kupotezea usajili dirisha dogo

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa timu ya Polisi Tanzania umesema hautafanya usajili wa mchezaji yeyote katika kipindi cha dirisha dogo linalotarajiwa kufunguliwa Desemba 15, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, baada ya kumalizika mechi yao dhidi ya Coastal Union iliyopigwa Uwanja wa Uhuru, Kocha Mkuu wa Polisi, Malale Hamsini, alisema kutokana na kuwa na kikosi kipana hana mpango wa kufanya usajili katika kipindi hicho.

"Tuna wachezaji wengi hapa sasa, mikataba yao ni ya muda mrefu, hivyo kama ni kusajili lazima tuwaache hawa tulionao na kutafuta wengine na kama ndivyo tukiwaacha lazima tuwalipe na tunayemfuata pia anatakiwa kulipwa na mara nyingi anayekuja hana tofauti na aliyeondoka," alisema kocha huyo.

Alisema kikubwa wanapambana kufanyia kazi udhaifu uliojitokeza kwa wachezaji wao hususan kukosa utulivu kwenye safu ya ushambuliaji.

## Kocha Malindi aahidi makubwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kuizamisha timu ya Polisi kwa mabao 2-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu Zanzibar uliopigwa Uwanja wa Amaan juzi, Kocha Mkuu wa Malindi FC, Mohammed Badru Juma, mbali na kuwashukuru wachezaji wake kwa kujituma katika mechi zote mbili walizocheza hadi sasa, amesema lengo lake ni kurejesha hadhi ya timu hiyo.

Badru alisema wachezaji wake walionyesha kiwango kizuri katika mechi hiyo ya pili tofauti na iliyopita, hivyo kwake yeye ni moja ya mafanikio wakati huu akitaka kuhakikisha hawapotezi mechi zao za nyumbani na zile za ugenini.

"Lengo langu ni kuona timu ya Malindi inarejesha heshima yake ya miaka iliyopita, hivyo lazima tuwe na kikosi bora chenye kucheza kwa malengo, hii itasaidia hata kuvuta watazamaji wengi uwanjani," alisema

Mabao ya Malindi katika mechi hiyo yalifungwa na Massat Kassim dakika ya 46 na Nassor Mattar dakika ya 59, wakati matokeo hayo yanaifanya Polisi sasa kupoteza mechi zote mbili za mwanzo kwenye Ligi Kuu msimu huu.

# NI WAKENYA TENA ROCK CITY MARATHON, RC ATOA NENO

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI msimu wa 11 wa mbio za Rock City Marathon ukihitimishwa kwa washiriki kutoka nchini Kenya kutamba kwenye mbio hizo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, amesema idadi kubwa ya washiriki kutoka ndani na nje ya nchi umekuwa na faida kubwa kiuchumi katika mkoa huo.

**Rock City Marathon msimu wa 11 zilihusisha mbio za Km 21, Km 10 na kilometa tano ambapo washiriki takriban 3,000 kutoka ndani na nje ya nchi walishiriki zikiwamo klabu za wakimbiaji kutoka mikoa mbalimbali, mashirika na taasisi, viongozi wa serikali, watu wenye ualbino na watoto, hivyo kuzifanya kutajwa kuwa miongoni mwa mbio kubwa nchini zikiwa na lengo la kukuza vipaji vya mchezo huo sambamba na kutangaza utalii wa ndani hususan Kanda ya Ziwa.**

Katika mbio za Km 21, upande wa wanaume ilishuhudiwa mwanariadha kutoka Kenya, Edward Kibet akiibuka mshindi wa kwanza akitumia muda wa saa 1:04:52 akifuatia na Mkenya mwenzake, Bernard Msau aliyetumia muda wa saa 1:04:55 huku nafasi ya tatu ikishikwa na Mtanzania Mathayo Sombi, akitumia muda wa saa 1:06:11.

Kwa upande wa wanawake pia ilishuhudiwa mwanariadha kutoka Uganda, Doreen Chemuthi, akiibuka mshindi baada ya kutumia muda wa saa 1:15:06, akifuatiwa na Mkenya Nesphine Teplenting aliyetumia muda wa saa 1:15:35, huku pia nafasi ya mshindi wa tatu ikishikiliwa na Mkenya Cecilia Wayda, akitumia muda wa saa 1:15:49.

Katika mbio hizo za wanawake nafasi ya pili hadi ya tisa zilishikiliwa na wanariadha kutoka Kenya huku Mtanzania Angelina Tsere akifanikiwa kushika nafasi ya kumi kwa kutumia muda wa saa 1:26:56 akifutiwa na Mtanzania mwingine Sara Hhiiti aliyetumia muda wa saa 1:26:56

Kadhalika, katika mbio hizo ilishuhudiwa mwanariadha wa Kimataifa kutoka Tanzania, Alphone Simbu, akishindwa kutamba kwa kile alichoeleza kuwa ushiriki wake kwenye ni mwanzo wa kujiandaa ili aweze kufanya vizuri kwenye mbio za kimataifa baada ya kutofanya mazoezi kwa muda mrefu kutokana na kusumbuliwa na majeraha.

Akizungumza wakati wa kilele cha mbio hizo zilizofanyika kwenye viunga vya jengo la Biashara la Rock City Mall jijini Mwanza, RC Mongella alionyesha kuridhishwa na kasi ya ukuaji wa mbio hizo akibainisha kuwa ongezeko la washiriki katika mbio hizo limekuwa likileta tija katika uchumi wa mkoa huo sambamba na kutangaza utalii wa Kanda ya Ziwa.

"Ukuaji huu unaoshuhudiwa katika mbio hizi ni ishara tosha kuwa zitakuwa ni moja ya mbio kubwa sana si tu hapa nchini bali pia kimataifa. Naamini tutaendelea kupokea wageni wengi zaidi wakiwamo watalii watakaokuja pia kutembelea vivutio vya utalii tulivyo navyo Kanda ya Ziwa," alisema.

Zaidi aliwapongeza wadau mbalimbali walioshiriki kufanikisha mbio hizo wakiwamo Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) cha Mwanza, Kampuni za TIPER, Magare Company Ltd, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), KCB Bank, Kampuni ya Ulinzi ya Garda World, CF Hospital, Bugando Hospitali, Azam Bakhresa Group kupitia maji ya Uhai, Pepsi, Vituo vya TV vya Azam na ITV pamoja na vyombo vyote vya habari kwa kuzitangaza vema mbio hizo.




Meneja Uhusiano wa Kampuni ya Kuhifadhi Mafuta ya TIPER, Emmanuel Kondi (kulia), akikabidhi zawadi kwa mshindi wa kwanza wa mbio za Km 21 za Rock City Marathon, mwanariadha kutoka Kenya, Edward Kibet (katikati) alishika nafasi ya kwanza kwa kutumia muda wa saa 1:04:52 kumaliza mbio hizo, zilizofanyika mwishoni mwa wiki jijini Mwanza. Wengine ni washindi wa pili na wa tatu wa mbio hizo. **MPIGAPICHA WETU**

# *Romeo azindua mafunzo ya kuogelea kwa watoto*

**Na Mwandishi Wetu**

MWOGELEAJI chipukizi nchini, Romeo Asubisye, amezindua programu ya mafunzo kwa waogeleaji wa shule za msingi mkoani Dar es Salaam yenye lengo la kuutangaza mchezo huo na pia kutoa mbinu za kujikinga na majanga ya maji.

Programu hiyo iliyopewa jina la "Dar Largest Swimming Lesson" ilizinduliwa Jumamosi kwa wanafunzi mbalimbali kutoka shule tofauti za msingi mkoani Dar es Salaam kushiriki na kuanza mafunzo hayo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Romeo alisema ameamua kuanzisha programu hiyo kama sehemu ya kutafuta vipaji miongoni mwa watoto ambao kwa namna moja au nyingine, wanashindwa kupata mafunzo hayo kutokana na changamoto mbalimbali.

Alisema mafunzo hayo yanatolewa bure na mipango yao ni kufanyika mara moja kila mwaka huku mipango ya mbioni ikiwa ni kuendesha mafunzo hayo kwa kila mwezi.

"Mimi nimejifunza kuogelea kutokana na sapoti kutoka kwa wazazi wangu, naomba wazazi kuwaruhusu watoto wao kujifunza kuogelea ili kujua vipaji vyao na vile vile kupata nafasi ya kujilinda na majanga ya maji.

"Hivi karibuni, familia nyingi ziliathirika na mafuriko na baadhi ya watu kupoteza maisha kutokana na kusombwa na maji. Lakini kama wangekuwa wanajua kuogelea, wasingeweza kupoteza maisha yao. Nimeona changamoto hiyo na ndiyo maana nimeamua kuanzisha mafunzo haya," alisema Romea.

Alisema mbali ya yeye kuwa miongoni mwa watoa mafunzo, pia makocha wa timu ya Champion Rise watakuwa wanashiriki katika mafunzo hayo ambayo katika uzinduzi, yalidhaminiwa na Kampuni ya Pepsi.

"Nawapongeza makocha wa klabu ya Champion Rise kwa kujitolea kuniunga mkono katika mafunzo haya, naamini tutafikia malengo yetu," alisema.

# Michezo

Jumanne Desemba 1, 2020

Nipashe




Aubameyang sasa ampa hofu Arteta UKURASA 22

MSITU...



Mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi, akipata wakati mgumu kuipenya ngome ya Osasuna kutokana na kuzingirwa na 'msitu' wa mabeki wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 kwenye mechi ya LaLiga iliyopigwa Uwanja wa Nou Camp juzi. **HABARI UK. 20**

## Kaseke: Yacouba ananipa mabao

**Na Adam Fungamwango**

WINGA mwenye kasi wa Yanga, Deus Kaseke, amesema huenda akafunga mabao mengi zaidi kama akiendelea kupangwa sambamba na straika raia wa Burkina Faso, Yacouba Songne kutokana na kumjulia jinsi ya kumpenyezea pasi za mwisho.

Kaseke amefunga kwenye mechi mbili mfululizo wakati Yanga ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Azam na JKT Tanzania, pasi zote zikitokea kwa Yacouba, jambo ambalo amelielezea kuwa 'Mbukinabe' huyo ametambua mikimbio yake, lakini pia hata yeye amekuwa akijipanga vema anapoona mchezaji huyo yupo kwenye nafasi nzuri ya kutoa pasi.

"Pacha yetu ni nzuri, akiwa na mpira ananitazama niko wapi ili apenyeze pasi, na mimi pia huwa namwangalia na kutafuta 'shimo' ambalo naweza kuupata mpira na kweli unaona anauachia mpira, anafunga," alisema.

Alisema kama ataendelea kucheza na Yacouba na kwa sababu kila mmoja ameshamfahamu mwenzake anafanya nini na wakati gani, basi anaweza kufunga mabao mengi zaidi kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Pointi sita ambazo Kaseke ameipa Yanga, dhidi ya Azam FC na JKT Tanzania, zimeiwezesha timu hiyo kukaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 31.

# Sven: Bado dakika 90 CAF

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

## ●●● Asema kazi ipo kwa Mkapa Jumamosi, wanasa mbadala wa Fraga kutoka Ligi Kuu Misri, lakini...

PAMOJA na kuonyesha kufurahishwa kwa ushindi wa bao 1-0 walioupata nchini Nigeria dhidi ya Plateau United juzi, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema kamwe hawapaswi kubweteka kwa matokeo hayo kwa kuwa bado hawajamaliza kazi waliyoianza.

**Simba ilianza vema mechi yake ya raundi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ikiwa katika Uwanja wa Jos mjini Jos, Nigeria, shukrani zikimwendea kiungo Clatous Chama baada ya kuitendea haki kazi nzuri iliyofanywa na winga Luis Miquissone kwa kuifungia timu yake bao hilo pekee katika dakika ya 53.**

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi hiyo, kocha huyo raia wa Ubelgiji alisema mchezo huo ulikuwa mgumu sana kutokana na wapinzani wao kutumia nguvu na mbinu mbalimbali kutafuta bao la mapema, lakini anawapongeza wachezaji wake kwa sababu dakika zote 90 walizuia vizuri.

"Nafikiri tunatakiwa kuwa na furaha sana kwa ushindi huu. Matokeo mazuri, lakini bado hatujamaliza kwa sababu tuna dakika zingine 90 za mchezo. Kuhusu mechi ni kwamba timu hii imenishangaza kidogo. Sikutegemea kama watacheza hivi, wanatumia nguvu, kasi na kutokana na hilo, ilibidi kipindi cha pili nibadilishe mbinu kuendana na kasi yao na kweli ilifanikiwa," alisema kocha huyo.

Sven alisema matokeo yaliyopatikana ni mtego kwao, kwani watalazimika kuhakikisha wanafanya vema kwenye mechi ya marudiano wakiwa nyumbani Tanzania.

Hata hivyo, kocha huyo ameonyesha kufurahishwa na kiwango cha uzuiaji mashambulizi kwa wachezaji wake ambacho kinazidi kukua siku hadi siku.

"Leo nimeona timu yangu ikiwa vizuri kwenye kuzuia, hali hii ni nzuri kwa maendeleo ya baadaye ya kikosi chetu kwenye mechi na michuano mbalimbali inayofuata," alisema.

Simba itarudiana tena na Plateau United Jumamosi ijayo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam ikiwa inahitaji sare yoyote ama ushindi ili kutinga raundi ya kwanza, na endapo itafanikiwa itakutana na mshindi wa jumla kati ya Costa do Sol ya Msumbuji ama FC Platinum ya Zimbabwe ambayo katika mechi ya awali nayo ilishinda kwa mabao 2-1 ugenini.

Wakati huo huo, taarifa zilizolifikia Nipashe jana kutoka ndani ya chanzo cha uhakika cha klabu ya Simba, zimeeleza kuwa wawakilishi hao wa nchi kimataifa na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, wapo kwenye mazungumzo na kiungo mkabaji wa timu ya Taifa ya Uganda na Klabu ya Tanta ya Misri, Taddeo Lwanga ili kuimarisha kikosi chao kuelekea usajili wa dirisha dogo llinalotarajiwa kufunguliwa Desemba 15, mwaka huu.

Kwa mujibu wa chanzo hicho, Lwanga ndiye atakayepewa viatu vya Mbrazil Gerson Fraga ambaye atakuwa nje ya uwanja kwa msimu mzima kutokana na kusumbuliwa na majeraha.

Mtoa habari huyo alisema Lwanga yupo hapa nchini kuisikilizia ofa ya Simba baada ya kuvunja mkataba na klabu yake ya Misri, huku akishindwa kuiweka wazi sababu ya kuvunja mkataba na Tanta ambayo alisaini msimu wa 2019.

"Tayari yupo hapa nchini kwa ajili ya mazungumzo baada ya kuvunja mkataba wake na klabu hiyo ya Ligi Kuu Misri, lakini ametueleza kuwa ana ofa nyingi nje ya Tanzania, ila anatoa kipaumbele kwetu baada sisi kuwa wa kwanza kumfuata," kilieleza chanzo hicho.

Alisema Kamati ya Usajili inaendelea na mchakato huku wakisubiriwa wajumbe wengine ambao wanawasili leo wakitokea Nigeria, pamoja na timu.

Kwa upande wa mchezaji na kocha wa zamani wa Simba, Talib Hilal, akitoa maoni yake kuhusu kikosi cha timu hiyo, alisema hawana haja ya kuongeza wachezaji wengi zaidi ya kutafuta mbadala wa Fraga.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042